SUPA JACKPOT
TZS. 1,099,164,188
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Watu** 500 wawekwa karantini ugonjwa wa Marburg

UKURASA 3


TESA
TEKNOLOJIA
Kifuu kilivyo mbadala wa zebaki migodi ya dhahabu

UKURASA 11

Nipashe
Jumatano Aprili 5, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581271
The Guardian digital
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Majaji wastaafu wataka kupunguzwa mamlaka wakuu mikoa, wilaya

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 4
**SPIKA ASHAURI MAGARI KURUHUSIWA USIKU**
SPIKA wa Bunge, Dk.Tulia Ackson, ameshauri serikali kulitazama upya suala la kuzuia magari ya abiria kutembea usiku...

UKURASA WA 4
**KAYA 20 ZAKOSA MAKAZI MUSOMA**
MVUA zinazoendelea kunyesha zimesababisha kaya 20 katika Kijiji cha Kusenyi, Kata ya Suguti wilayani Musoma...

UKURASA WA 7
**SIMBACHAWENE ASISITIZA DHAMIRA UTUMISHI BORA**
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene ameeleza...

## Bunge lampongeza Rais kwa kuimarisha demokrasia, diplomasia

UKURASA 3





“Tumekazania sana kumwangalia mhalifu na adhabu kwao na kumsahau mwathirika ni lazima sasa tuwe na mfumo wa fidia wa kuwasaidia hasa kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia.

**Prof. Kabudi**

“Tumegusia haya mamlaka ambayo wakuu wa mikoa na wilaya wanayatumia eeh kamata watu, muweke ndani, ondoka naye na kadhalika... maagizo hayo yatolewe kwa maandishi ili kama mtu ataona ana haki ya kushtaki, kuwe na ushahidi.

**Jaji Mihayo**



Mikono ya Elizabeth Mathias baada ya kuchomwa kwa maji ya moto. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Baba adaiwa kumchoma mtoto madai kuiba 5,000/-

UK. 2

**MICHEZO** **MAYELE: NINA DENI LA KUTETEMA SIMBA** UK.24 **KATUNI** UK.6




Watumishi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), wakisafisha miundombinu ya majitaka katika maeneo mbalimbali ya jijini humo jana, inayoziba kutokana na wananchi kutupa taka. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Majaji wataka kupunguzwa mamlaka za Ma-RC,Ma-DC

**Na Restuta James**

CHAMA cha Majaji Wastaafu Tanzania (TARJA) kimependekeza wakuu wa mikoa na wilaya kupunguziwa mamlaka ya kuweka watu ndani huku kikipendekeza vifo vyenye utata vichunguzwe na mahakama.

Aidha, kimependekeza utaratibu wa plea bargaining utathminiwe kwa kuwa watu wanaoingia kwenye mpango huo ni wale ambao wameshanyanyaswa kwa kuwekwa mahabusu muda mrefu, hivyo wanakubali masharti hayo ili kukwepa mazingira ya magereza.

Wakati majaji wastaafu wakipendekeza hivyo, Waziri wa zamani wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi, amependekeza waathirika wa uhalifu wa kijinai wakiwamo waliobakwa, walipwe fidia na kupewa ushauri wa kisaikolojia badala ya mifumo ya hakijinai kuwatumia tu kama mashahidi mahakamani.

Jaji Mihayo na Prof. Kabudi walitoa mapendekezo hayo jana jijini Dar es Salaam mbele ya Tume ya Kurekebisha Mifumo ya Hakijinai inayoongozwa na Jaji Mkuu Mstaafu, Mohammed Othman Chande.

Jaji Mihayo alisema wakuu wa mikoa na wilaya wamekuwa na kasumba ya kutoa amri ya kukamata watu, hivyo amependekeza amri hiyo isiwe kauli ya mwisho, bali mtuhumiwa apewe haki ya kumshtaki kiongozi huyo ikiwa atakamatwa kwa uonevu.

"Tumegusia haya mamlaka ambayo wakuu wa mikoa na wilaya wanayatumia eeh kamata watu, muweke ndani, ondoka naye na kadhalika. Tumependekeza kwamba ili yaweze kufuatiliwa na kuwa maagizo hayo yatolewe kwa maandishi ili kama mtu ataona ana haki ya kushtaki, kuwe na ushahidi," alisema.

"Tumependekeza kuhusu hizi kamati za ulinzi na usalama, kumekuwa na kutoeleweka kwa kazi yake. Kazi yake si kukamata watu wala kuagiza watu kukamatwa bali kuangalia hali ya mkoa au wilaya kiusalama," alisisitiza.

Alisema kamati hiyo ikibaini kuna shida ya usalama inapaswa kuwasiliana na Jeshi la polisi ambalo ni mjumbe, ili kudhibiti matukio ya uhalifu na si vinginevyo.

## 'PLEA BARGAINING'

"Plea bargaining' kama ilivyo si haki kwa sababu haijaeleza itafanyika kwa wakati gani na haina usawa. Unakuta mtu amekaa ndani kwa kosa la uhujumu uchumi, yuko ndani miaka sita halafu anaambiwa aende kwenye plea bargaining ana uhuru wa kufanya hivyo huyo?" alihoji.

Jaji Mihayo alisema kinachotakiwa ni kuruhusu 'plea bargaining' kufanyika kwa uwazi badala ya kutumia utaratibu huo kuumiza watu. Pia alipendekeza Mwendesha Mashtaka wa Serikali (DPP) aondolewe mamlaka ya kunyima watuhumiwa dhamana.

"Uhuru wa mtu ni wa msingi na ni kiini cha ubinadamu, hivyo sheria yoyote inayomnyima mtu uhuru iangaliwe kwa makini," alisema.

## VIFO POLISI, MAGEREZA

Kuhusu vifo vyenye utata, TARJA imependekeza uchunguzi wa matukio hayo ufanywe na mahakama ili kuondoa sintofahamu.

Alisema kulikuwa na sheria ya inquest (uchunguzi) inayotoa mamlaka ya kuchunguza sababu za kifo kwa vifo vyenye utata, akitaka ombi la uchunguzi litolewe na hakimu au jaji ili kutoa haki kwa walalamikaji.

"Mtu akifariki (dunia) gerezani, kituo cha polisi au mahali penye wasiwasi, kifo hicho kinachunguzwa na hakimu. Akijiridhisha kuna mtu anapaswa kushtakiwa basi anaagiza mtu fulani au kundi fulani wakamatwe na kushtakiwa. Hamtii mtu hatiani bali atapendekeza watuhumiwa wafunguliwe mashtaka. Hivi ndivyo ilivyokuwa huko nyuma.

"Ndiyo maana unaona mtu anapofariki dunia polisi wanasema amejinyonga. Ndugu wanakataa. Kama ingefanyika 'inquest' angejulikana nani amehusika. Hakimu angefika mahali na kusema hakufa kifo cha kawaida, aliuawa au aliteswa hadi akafa," alisema.

## WAATHIRIKA UHALIFU

Kuhusu waathirika wa uhalifu, Prof. Kabudi alisema kwa hali ilivyo sasa, haitazamwi sana na sheria badala yake mifumo imemlenga zaidi mhalifu.

"Tumekazania sana kumwangalia mhalifu na adhabu kwao na kumsahau mwathirika ni lazima sasa tuwe na mfumo wa fidia wa kuwasaidia hasa kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia, kubakwa na kudhalilishwa," alisema.

Alisema mwathirika wa uhalifu anapaswa kusaidiwa kitabibu ili kutoka kwenye tatizo alilo nalo. Alisema amependekeza pia mafunzo ya ufundi kwa wafungwa na fursa ya masomo kwa watu wanaokutwa na hatia wakiwa na umri mdogo.

Katika eneo hilo, alipendekeza pia magereza ya wazi kwa wafungwa wataalam kama madaktari na wahandisi, ambao wametiwa hatiani kwa makosa madogo ili waendelee kufanyakazi.

Alisema amependekeza pia maboresho ya sheria nyingi mbalimbali pamoja na muundo wa taasisi zinazoshughulikia mifumo ya hakijinai likiwamo jeshi la polisi.

Prof. Kabudi alipendekeza pia kiundwe chombo kitakachosikiliza wananchi ambao wataona wamenyanyashwa na taasisi zinazosimamia hakijinai, hususani matumizi mabaya ya madaraka yanayofanywa na baadhi ya maofisa wa vyombo hivyo.

Alisema taasisi zinazoshughulikia mfumo wa hakijinai zinapaswa kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Ibara za 9, 12 na 13 za Katiba, zinazosisitiza heshima na utu wa kila mtu bila kujali ni mhalifu au mwathirika wa uhalifu.

# Baba adaiwa kumchoma mikono mwanawe madai kaiba 5,000/-

**Na Marco Maduhu,** GEITA

BABA mzazi anyefahamika kwa jina la Mathias Daudi, mkazi wa kijiji cha Nyarugusu, wilaya ya Geita, amedaiwa kumchoma mtoto wake kwa kuingiza mikono yake kwenye sufuria ya maji ya moto iliyokuwa jikoni kwa madai ya kuiba Sh. 5,000 kwa jirani.

Mtendaji wa Kata ya Nyarugusu, Lusekelo Mwaikenda, akielezea tukio hilo jana, alisema lilitokea Aprili Mosi, mwaka huu, majira ya saa 1:00 jioni.

Alimtaja mtoto huyo kuwa ni Elizabeth Mathias (10), mwanafunzi wa darasa la nne katika Shule ya Msingi Zahanati, Nyarugusu.

Mwaikenda alisema baada ya mtoto huyo kuiba fedha hiyo, alimpelekea baba yake akimwambia ameiokota na kisha kupangiwa matumizi ya familia.

"Mtoto huyo alipokwenda kununua vitu vya matumizi ya nyumbani kwa pesa hiyo, aliporudi nyumbani alimkuta jirani yao akimsema kuwa amemwimbia Sh. 5,000, ndipo baba yake mzazi akaanza kumtembezea kichapo na kisha kumloweka mikono yake yote miwili kwenye sufuria yla maji ya moto iliyokuwa jikoni," alisema Mwaikenda.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita, Alex Herman, alisema baada ya kupata taarifa za mtoto huyo kufanyiwa ukatili na baba yake, walimfuatilia kwa ukaribu na kisha kumkamata na kumpelekea polisi ili hatua za kisheria zichukue mkondo wake.

"Tunaishukuru timu ya wanasheria watetezi wa mazingira kwa vitendo (LEAT) kwa kutoa elimu ya kutoa taarifa za ukatili kwa mabaraza ya kata, ndiyo hao walitoa taarifa juu ya tukio la mtoto huyu na pia LEAT wamemtoa mtoto huyo Nyarugusu na kumleta hapa Hospitali ya Mkoa wa Geita na anaendelea kupatiwa matibabu," alisema Herman.

Pia alisema mtoto huyo akipona hawatamrudisha nyumbani kwa baba yake, bali watamtafutia mahali pengine pa kuishi ikiwamo kwenye nyumba za kulea watoto kwa sababu tayari ameshaathirika kisaikolojia.

Ofisa wa LEAT, Valeria Macha, alisema walipokea taarifa juu ya tukio la mtoto huyo kuchomwa maji ya moto, ndipo wakawasiliana na Maofisa Maendeleo wa Geita na walipofika eneo la tukio walimkuta mtoto akiwa katika hali mbaya ndipo wakamchukua na kumpeleka Hospitali ya Mkoa Geita kwa matibabu zaidi.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Geita, Sophia Jongo, alisema taarifa za tukio hilo bado hajazipata kwa sababu yuko nje ya ofisi.

HABARI KITAIFA



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kupungua kwa ugonjwa wa Marburg nchini. Kushoto ni Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Watu 200 wawekwa karantini ugonjwa Marburg

**Na Halfani Chusi**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema watu 200 waliokuwa wamewekwa kizuizini kwa ajili ya uangalizi dhidi ya mlipuko wa ugonjwa wa Marburg, 35 kati yao wameruhusiwa baada ya kukaa siku 21 na kuthibitika hawana maambukizi.

Ugonjwa huo uliibuka Machi 21, mwaka huu, na kusababisha vifo vya watu watano na wagonjwa watatu, ambao mmoja kati yao ameruhusiwa baada ya kutibiwa na kupona huku wengine hali zao zikiendelea kuimarika.

Waziri Ummy aliyasema hayo jana Dar es Salaam kwenye mkutano na waandishi wa habari, alipokuwa akitoa taarifa juu ya mwenendo wa ugonjwa huo akisisitiza kuwa mbali na visa hivyo hakuna vingine.

Alisema katika wagonjwa watatu waliokuwa kwenye matibabu mpaka sasa wamefanikiwa kumruhusu mgonjwa mmoja wa kiume mwenye umri wa miaka 26, akiwa amepona na wengine wawili waliolazwa wanaendelea vizuri mmoja kati yao ni mtumishi wa afya.

"Nimatumaini yangu jamii haitamtenga. Tumempima zaidi ya mara tatu hana tena ugonjwa huo yuko vizuri, ninaomba familia yake ndugu na majirani, wasimtenge na badala yake wampokee na kuzungumza naye yupo vizuri," alisihi.

Waziri Ummy aliwapongeza wahudumu wa afya mkoani Kagera kwa kuwahudumia wagonjwa bila uoga wala unyanyapaa akisisitiza kuwa bado wanaendelea kuwafuatilia watu walio tangamana kwa ajili ya kuwaepusha kuambukiza wengine.

"Kwenye kudhibiti maambukizi haya, tunaendelea na kazi ya kufuatilia watu waliotangamana na wagonjwa. Kama wanafamilia na watumishi wa afya ambao jumla yao ni zaidi ya 200 na tayari watu 35 wametoka kizuizini baada ya kukaa siku 21 za uangaliazi bila kuonyesha dalili zozote hivyo tumewaruhusu kurejea kwenye familia zao.

"Hii ni ishara nzuri kuwa maambukizi ya virusi hivyo, yamedhibitiwa kwa ufasaha hata hivyo, serikali inahimiza wananchi wote kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya maambukizi mapya ya ugonjwa huo," alisema.

Alitahadharisha kuwa kama kutakuwa na mgonjwa kwenye jamii mwenye dalili za homa kali, kutapika, kuharisha, kutokwa damu, na kuishiwa nguvu wananchi wapige simu bure kupitia namba 199, ili kupata huduma za awali kutoka kwa wataalamu wa ugonjwa huo.

"Ikigundulika ana ugonjwa huo, atapelekwa katika vituo tulivyovitenga kwa ajili ya uangaliazi. Kwa hiyo tuepuke kugusa majimaji yanayotoka kwa mgonjwa kama jasho, mate, machozi, kinyesi pamoja na kuzingatia unawaji mikono kwa maji tiririka yaliyo safi kwa sabuni, kuosha matunda na kula vyakula vilivyopikwa kikamilifu.

"Ninasisitiza hata tutakapo mtoa mgonjwa wa mwisho tunapaswa kuendelea kuchukua tahadhari mpaka pale tutakapo jiridhisha kuwa ugonjwa huo umekwisha tuendelee kuzingatia kanuni za afya na maelekezo ya wataalamu wetu," alisema.

Vilevile aliwashukuru wadau mbalimbali wanaounga mkono juhudi za serikali kwenye sekta hiyo ikiwamo, kituo cha udhibiti wa magonjwa cha Marekani na washirika wengine wa afya na asasi zisizo za kiserikali.

"Ninawahakikishia Watanzania kuwa Bukoba ni salama, Kagera ni salama na Tanzania iko safi, hivyo tuendelee na shughuli zetu. Bila shaka hata kwenye kata ambazo ugonjwa huu ulianzia nimefika na kote kupo salama," alisema.

# Bunge lampongeza Rais kwa kuimarisha demokrasia, diplomasia

**Na Godfrey Mushi,**
DODOMA

BUNGE limepitisha azimio la kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuimarisha demokrasia nchini na kukuza diplomasia ya uchumi, huku likitaja mambo manne yaliyomwezesha kuyafikia mafanikio makubwa na kuwa mwanadiplomasia namba moja wa uchumi.

Azimio hilo lilipitishwa jana bungeni jijini hapa baada ya Mbunge wa Biharamulo (CCM), Ezra Chiwelesa, kuwasilisha taarifa ya kuwaomba wabunge kuridhia Rais Samia Suluhu Hassan kupongezwa kutokana na kuimarisha demokrasia na kukuza diplomasia ya uchumi.

Alisema katika mkutano wake wa na 11, ulioanza jana, Bunge linaazimia kwa dhati na kauli moja, kumpongeza kwa kuimarisha demokrasia nchini, kukuza diplomasia ya uchumi na kumuunga mkono katika majukumu yake ya kazi ya Rais.

Azimio hilo liliwasilishwa Bungeni, kwa mujibu wa Kanuni ya 61 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 na kwa mujibu wa Chiwelesa, miongoni mwa mambo muhimu yaliyochangia kuimarika kwa demokrasia ni pamoja na uamuzi wa Rais Samia kuruhusu shughuli za siasa hasa mikutano ya hadhara kufanyika nchini kote.

"Uamuzi huu, umefufua na kuimarisha shughuli za siasa nchini kwani vyama vya siasa vimepata fursa ya kunadi sera zao na kutoa mawazo mbadala ambayo yataisaidia serikali kutekeleza huduma za kijamii na kiuchumi hususani masuala yanayogusa maendeleo ya wananchi.

"Kuanzisha vikao vya maridhiano ya kisiasa miongoni mwa vyama vya siasa nchini, ili kuhakikisha kunakuwepo mahusiano mema miongoni mwa makundi ya kisiasa yaliyokuwa yakihasimiana," alisema na kuongeza:

"Kuanzisha mchakato wa kufanya marekebisho ya kimfumo na kisheria yanayoongoza shughuli za kisiasa; na kudumisha misingi ya amani na mshikamano miongoni mwa Watanzania; Limo pia, kuridhia kuundwa kwa kikosi kazi cha kufanyia kazi masuala yanayohusu demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini, ambapo lengo kubwa la kikosi kazi hicho, lilikuwa ni kupendekeza namna bora ya kutekeleza haki ya vyama vya siasa, ikiwemo kuwepo na uwanja sawa wa

kufanya shughuli za kisiasa bila ya kukiuka sheria na maadili ya nchi yetu."

Aidha, katika azimio hilo, Chiwelesa alisema katika kipindi hicho, Watanzania wameshuhudia nchi ikipata mafanikio kama kuongezeka kwa masoko ya bidhaa zinazozalishwa nchini katika masoko ya nje na kuimarika kwa uhusiano wa kimkakati na kampuni za kimataifa unaolenga kuwekeza katika sekta za uzalishaji, ili kuchochea ukuaji wa uchumi.

Mambo mengine yaliyomo katika azimio hilo ni kumpongeza Rais Samia, kwa kuwezesha upatikanaji wa misaada na mikopo ya masharti nafuu kutoka kwenye taasisi za fedha duniani, ambayo kwa kiasi kikubwa imesaidia kuboresha shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwemo elimu, miundombinu, afya na maji.




# Lema awanyooshea kidole viongozi dini kuhusu haki

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MBUNGE wa zamani wa Arusha na Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasi na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema, amesema kukosekana kwa haki kwa wananchi kumechangiwa na baadhi ya viongozi wa dini kushindwa kutekeleza majukumu yao ya kuisaidia jamii kupata amani kwa wakati.

Lema pia amesema viongozi hao wanawajibu wa kuisaidia serikali kwenye utekelezaji wa majukumu ya kuwaletea wananchi maendeleo kwa kuanzisha miradi yenye tija na isiyo na madhara

Aliyasema hayo juzi katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika kata ya Marangu Mashariki, Moshi mkoani Kilimanjaro, uliokuwa na lengo la kuwashukuru wananchi kwa kuwapigia kura 2020 pamoja na kupokea matatizo.

Alisema taasisi hizo zilipaswa kuwa mstari wa mbele katika kuhubiri haki na amani ili kumaliza baadhi ya matatizo miongoni mwa jamii yakiwamo kuonewa, kupigwa, unyanyasaji na mporomoko wa maadili katika taifa.

"Wakati tunakua tuliamini viongozi wa dini wanafanya kazi ya haki sana. Tunavyozidi kuendelea kukua tunawaona vijana usiku na mchana wanahubiri neno haki, kazi ambazo zilipaswa zifanywe na kanisa na msikiti. Kwa bahati mbaya sana yako baadhi ya mambo ambayo wananchi wanalalamikia yangeweza kuamuliwa na taasisi za dini ingekuwa kazi ya Mungu inafanywa ipasavyo.

Leo hali ni mbaya sana, hakuna kabila lenye kiu na linatafuta maendeleo kama wachaga, lakini hakuna kabila linalorudi nyuma katika maadili kama wachaga, hii inaonyesha jinsi ambavyo hali ni mbaya na jitihada za haraka zinapaswa kuchukuliwa ili kunusuru hali hiyo," alisema Lema.

Akizungumzia suala la wananchi kukataa kufungiwa mita za maji, Lema aliishauri Wizara ya Maji kuhakikisha inakuja na mbinu mpya ya kuhakikisha hawawachaji gharama za maji wananchi hao na badala yake kuwawekea mkakati wa upandaji wa miti katika kila familia na kuwa na utaratibu wa kuikagua.

"Wakati umefika wizara na wataalamu wake kuja na mbinu mbadala ya kuhakikisha wanawahamasisha wananchi wote waishio chini ya Mlima Kilimanjaro hasa katika maeneo ya vyanzo vya maji, kuotesha miti zaidi ya 100 kila familia na kutunza, hii ingesaidia kuboresha uoto wa asili na kutunza mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi yanayoendelea hivi sasa.

"Kwa kufanya hivyo kutasaidia wananchi kuwa walinzi wa vyanzo vya maji pamoja na kutunza mazingira, pia migogoro ya uharibifu ya miundomonu haitakuwepo," alisema Lema.

Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA), Grace Kiwelu, alisema wananchi wanakabiliwa na matatizo mengi na kutafuta watu wakuwasemea bungeni, ili yaweze kutatuliwa kwa wakati na si mwakilishi anaye lala bungeni.

Aidha, Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Kilimanjaro, Michael Kilawila, aliwataka vijana na wananchi ifikapo 2024 kujitokeza kwa wingi na kuingia kwenye nafasi za uongozi ili kuleta mabadiliko.

"Vijana ni taifa la leo na tunaona wanawake wakipewa nafasi wana uwezo wa kufanya mabadiliko na maendeleo, tunaomba wakati unapofika tujitokeze tuchukue fomu na kugombea nafasi za uongozi," alisema Kilawila.




Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Sayansi na Teknolojia, Dk. Amos Nungu, akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana, kuhusu Kongamano la Sayansi, Teknolojia na Ubunifu linalotarajiwa kufanyika Juni 14-16 mwaka huu. Kulia ni Mkurugenzi Menejimenti ya Maarifa, Mhandisi Samson Mwela. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## Kaya 20 zakosa makazi Musoma

**Na Mathias Marwa,** MUSOMA

MVUA zinazoendelea kunyesha zimesababisha kaya 20 katika Kijiji cha Kusenyi, Kata ya Suguti wilayani Musoma, kuharibiwa vibaya kutokana na maji ya Mto Suguti kuingia kwenye makazi ya wananchi.

Chanzo cha mafuriko kwenye nyumba hizo ni mto huo unaomwaga maji katika Ziwa Victoria kufurika kiasi cha kushindwa kuhimili maji kwenye mkondo wake, kisha kuingia kwenye mashamba na nyumba za wananchi.

Baadhi ya wananchi wakizungumza na Nipashe waliiomba serikali kuwasaidia msaada wa dharura wa chakula pamoja na hema za kujihifadhi kwa muda wakati wakishughulikia makazi yao.

Sondole Kuboja, mkazi wa kata hiyo na mfanyabiashara ya duka alisema mafuriko hayo yalikata mawasiliano ya barabara hali iliyowafanya wetembea kwa miguu pia kukwama.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Musoma Vijijini, Denis Ikwabe, aliliambia gazeti hili kuwa katika mafuriko hayo madhara yaliyotokea ni ya mazao ya chakula pamoja na makazi lakini hakuna majeruhi wala vifo.

Vitu vingine ni pamoja na vyombo vya ndani, mahindi, Mchele, magodoro na nguo hii ni kutokana na wananchi kuendesha shughuli za kilimo kando ya mto huo na kuharibu mfumo na mwelekeo wa maji katika eneo hilo," alisema.

Ikwabe aliiomba serikali kutoa pesa zilizokubaliwa kujenga barabara inayotoka Musoma yenye urefu wa kilometa 92, ili mifereji itakayotengenezwa iweze kupitisha maji hayo na kupunguza ukubwa wa tatizo.

"Tunaomba serikali ione uhitaji wa wananchi hawa kwa kipindi hiki kigumu kwa kwa kutoa msaada wa haraka wa chakula vifaa vya malazi na mahema ili kunusuru kaya hizi," alisema.

Kwa mujibu wa Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo, upepo huo uliokuwa wa kasi kubwa uliharibu mitumbwi 44 na mingine 167 iliyohitaji ukarabati. Mtumbwi mmoja unagharimu Sh. milioni 1.7 kutengenezwa.

# Spika Tulia ashauri magari kuruhusiwa kutembea usiku

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk.Tulia Ackson, ameshauri serikali kulitazama upya suala la kuzuia magari ya abiria kutembea usiku hasa kwenye maeneo ambayo usalama na miundombinu ni mzuri.

Ushauri huo aliutoa bungeni jana baada ya Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, kujibu maswali ya nyongeza ya Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Janeth Massaburi.

"Najiuliza magari ya abiria yanaruhusiwa usiku?," alihoji Spika huku Naibu Waziri Sagini akijibu kuwa yanaruhusiwa hadi saa sita usiku na kuna maeneo yamezuiwa kwa sababu ya matatizo ya kiusalama na miundombinu.

Sagini alisema eneo kama Tabora hadi Katavi ni hatari kutembeza gari usiku na wameshauriwa kupita maeneo hayo ikiwa bado mchana.

Kutokana na maelezo hayo, Spika Tulia alisema: "Hili jambo nilishawahi kulisemea mahali pengine. Ni vizuri serikali ilitazame kwa ujumla wake. Tunazuia magari ya abiria kutembea mwisho saa sita usiku kwa sababu ipi? Kwa sababu madereva ni wale wale wanaotuendesha sisi na wale wanaoendesha magari mengine ni masomo ni yale yale, kama kuna mahali kuna mapungufu yafanyiwe kazi.

"Suala la kuzuia abiria wanakaa hapo halafu gari linaondoka baada ya saa nne labda saa 10 au 11 usiku sijui tumezuia nini kipindi hiki ambacho serikali inafanya kazi kubwa ya kuboresha miundombinu ya barabara. Sasa zile barabara tunatengeneza kwa ajili gani kwa sababu yule abiria angekuwa na gari binafsi angetembea huo usiku kwa kuwa inabidi asubiri."

Dk. Tulia aliomba serikali kuliangalia suala hilo hasa kwenye maeneo ambayo usalama na miundombinu ya barabara ipo vizuri waruhusiwe watembee usiku.

Hata hivyo, Naibu Waziri Sagini alisema wamepokea ushauri huo utazingatiwa na kutoa maelekezo sahihi.

Katika maswali ya nyongeza, Mbunge Massaburi alisema moja ya sababu za ajali nyingi nchini ni wembamba wa barabara.

"Je, serikali haioni haja ya kuruhusu magari makubwa ya mizigo kutembea nyakati za usiku?, je, ni umri upi unaoruhusu kutoa leseni kwa madereva wa magari makubwa?,"alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alithibitisha taarifa za utafiti kuonyesha wembamba wa barabara unasababisha ajali na linafanyiwa kazi na watu wa uchukuzi na usafirishaji kwa kuwa ni wajumbe wa baraza la usalama barabarani.

"Kama mmeona Mbeya kule tunatanua barabara eneo ambalo imeonekana ni changamoto na suala la magari ya mizigo kutembea usiku sio suluhisho la kudumu, ili nchi ichangamke kibiashara hatuwezi acha kusafirisha muda wote na si usiku tu, kinachofanyika ni kusimamia sheria za usalama barabarani na kuboresha miundombinu ya barabara ili kuwa na usalama wakati wote," alisema.

Kuhusu umri, Sagini alisema umri wa dereva ni mtu mzima ambaye ana zaidi ya miaka 18 amefanya mafunzo na kufuzu vigezo vyote napewa leseni ya kuendesha magari.

**HABARI KITAIFA**

# Vijana wanaosafisha hifadhi ya Mikumi wasimulia wanavyokwepa simba, viboko

**Na Joseph Mwendapole,** MIKUMI



VIJANA wanaofanya usafi ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Mikumi, wamesimulia wanavyomudu kufanya shughuli hiyo kila siku bila kupata madhara ya wanyama wakali kama nyati, simba, viboko na mamba.

Walitoa simulizi hizo mwishoni mwa wiki walipotembelewa na wahariri wa vyombo vya habari baada ya mkutano ulioandaliwa na Chama cha Wanahabari wa Mazingira (JET) na mafunzo yanayofadhiliwa na Internews Earth Journalism Network East Africa.

Kwenye mahojiano na Nipashe, Mwenyekiti wa chama cha Mikumi Environmental Conservation Development (MECODE), Musa Buhaki, alisema hifadhi ya Mikumi imewapa ajira vijana wanaozunguka hifadhi hiyo kufanya usafi na imewapa elimu ya ikolojia ya namna ya kuwakwepa wanyama wakali.

Alisema kazi yao kubwa ni kusafisha kilomita 50 ya barabara inayokatisha ndani ya hifadhi hiyo kwa kuondoa vitu vyote visivyohusiana na mbuga.

Buhaki alisema imekuwa kawaida wasafiri kutupa vitu mbalimbali wanapopita kwenye hifadhi hiyo na kwamba wakati mwingine hata matairi ya magari ya akiba hudondoka bila wenyewe kujua.

Alisema wamekuwa wakigawanyika wawili wawili kila baada ya kilomita saba kwenye barabara hiyo na kwamba kuna wakati wanaitwa kuingia kwenye hifadhi kufanya usafi kama huo.

Kuna wakati, alisema wanaitwa kwenda kusafisha bwawa wanaloishi viboko na mamba ambalo mara kwa mara limekuwa likifunikwa na majani na wanyama hao kukosa hewa.

Alisema wamekuwa wakiingia kwenye bwawa hilo wakati viboko na mamba wakiwemo lakini wanasafisha bwawa na kutoka wakiwa salama kwani wanambinu za kiikolojia kuwakwepa wanyama hao.

"Ikolojia inafanyakazi kwa sababu bila ikolojia hata pale mbugani huwezi kukatisha tunachokifanya sisi unapoingia kwenye maji kiboko anataharuki na akija utaona mchirizi kwamba anakufuata unachotakiwa kufanya ni kuzama kwenye maji.

"Kwa sababu kwenye maji hawezi kufungua mdomo wake maji yataingia tumboni mwake na ndiyo maana akitaka kucheka anatoa mdomo juu ya maji kwa sababu hawezi kuachama majini," alisema Buhaki.

Aliongeza kuwa wakati mwingine wamekuwa wakitumia miti ya mianzi ambayo hupasuliwa katikati kwa kuipiga kwenye maji na kutoa sauti ambayo imekuwa ikiwakera na kuondoka majini.

"Siku ya kwanza kwenda kusafisha lile bwawa tulikuta viboko kama 60 siku ya pili tukawakuta kama 40 na wakaendelea kupungua kadri siku zinavyokwenda na tukafanya kazi zetu vizuri," alisema Musa.

Kuhusu mamba, alisema wamekuwa wakiyatibua maji mamba na viumbe wengine kama samaki wanakosa hewa hivyo kulazimika kwenda pembeni ya bwawa kutafuta hewa hivyo kuwapa nafasi ya kuendelea na usafi wao.

"Wanyama wenyewe hawapendi kero wakiona mmekuja mle siku ya kwanza kesho yake wakawaona wanaondoka zao na wakija tena kukagua wakakuta hampo wanarudi tena kwenye bwawa lao," alisema Musa

Alisema kwa upande wa barabara wamekuwa wakikutana na wanyama wakali kama simba na nyati lakini wamekuwa wakitumia mbinu za kiikolojia wanazofundishwa na hifadhi ya Mikumi kuwakwepa.

Alitoa mfano kuwa simba akishashiba hana madhara kwa binadamu na kwamba uzoefu unaonyesha kuwa simba hana kawaida ya kumdhuru binadamu kama hajamchokoza.

"Nyati ni mkorofi lakini wakiwa watatu kuendelea wanakuwa kama ng'ombe lakini wakiwa watatu kushuka chini hasa akiwa mmoja unapaswa kujihadhari naye kwa sababu anakosa kujiamini na anahisi unamuwinda.

"Ikitokea nyati anakukimbiza kimbia ukiwa kwenye barabara ya lami kwa sababu kwato zao haziwezi kuhimili anakuacha lakini ukiwa pembeni ya barabara atakukamata mara moja tu kwa sababu ndiyo maeneo yake," alisema na kuongeza:

"Wanyama wote wenye kwato hawana uwezo wa kukimbia mita 20 na kuendelea kwenye lami kwa sababu kwato zao zitatoboka na kutengeneza vidonda chini hali ambayo wanajua kwamba itahatarisha uhai wao kwani watashindwa kwenda kutafuta malisho.


# Bank of India (Tanzania) Ltd.

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)** *Relationships beyond banking*

**ISCLOSURES MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS, 2014 AND CONSUMER PROTECTION REGULATION, 2019**

**MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)**

**Service Charges (Exclusive of VAT and Government Levy on DigitalTransactions)**

**(The applicable VAT (Value added Tax) and Govt Levy on digital Transaction to be collected during the collection of service charges)**

**A. REMITTANCE – OUTWARD**

| Sr. No. | Item | Charge |
|---|---|---|
| **TISS Remittance** (Only for A/c holders – Not permitted for non a/c holders) | Remittance -TZS | TZS 10,000 |
| | Remittance -USD | USD 10 |
| **Other Outward Remittance** | 1USD up to 6,000 | USD 15 |
| | USD 6,001 – 10,000 | USD 30 |
| | Above USD10,000 | @ 0.35% Maximum USD 75 |
| Tracer Charges | Irrespective of Amount | USD 30 |
| Recall back funds charges | Irrespective of Amount | USD 30 |

**B. REMITTANCE – INWARD**

| Sr. No. | Item | Charge |
|---|---|---|
| (Only for A/c holders – Not permitted for non a/c holders) | From inside Tanzania | Free |
| | From outside Tanzania: as under | |
| | For Current /Overdraft Accounts | 0.35% of inwards remittance Minimum USD 18 Maximum USD 70. |
| | For Saving Accounts | |
| | USD 0 up to USD 100 | Free |
| | USD 101 up to USD 500 | USD 10 |
| | Above USD 500 | USD 18 |

**C. DEPOSIT AND RELATED SERVICES**

| Item | TZS A/c | USD A/c |
|---|---|---|
| **Saving Account :-** | | |
| Cash withdrawal per day –Free of charge, up to amount | TZS 25 Mn | USD 2000 |
| Cash withdrawal charges over USD 2,000 to USD 5000 per day | -- | 0.25% of withdraw amount |
| Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | -- | 0.60% of withdraw amount |
| Cash withdrawal charges over TZS 25 Mn per day | 0.10% of withdrawal amount | |
| Cash Deposit charges over USD 5,000 per day | -- | 0.60% of deposited amount |
| Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both for below and above USD 5,000) | -- | 12% (Min USD 1) of the aggregate small currency amount |
| **Current Account:-** | | |
| Cash withdrawal per day –Free of charge, up to amount | TZS 25 Mn | USD 5000 |
| Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | -- | 0.60% of withdrawal amount |
| Cash withdrawal charges over TZS 25.00 Mn per day | 0.15% of withdrawal amount | -- |
| Cash deposit charges over USD 10,000 per day | | 0.60% of deposit |
| **Maintenance of minimum balance: -** | | |
| For Saving Account-Without Cheque Book Facility | TZS 50,000 | USD 50 |
| With Cheque Book Facility | TZS 200,000 | USD 200 |
| For Current Account | TZS 200,000 | USD 200 |
| **Minimum balance charges (in case of non-maintenance of minimum balance)** | | |
| Saving Account - Without cheque book | TZS 900 p.m | USD 4 p.m |
| With cheque book | TZS 3600 pm | USD 15 p.m |
| Current Account- | TZS 20,000 p.m | USD 15 p.m |

**D. Other Common Charges**

| Item | Charges | |
|---|---|---|
| | **TZS A/c** | **USD A/c** |
| Stop Payment Instructions | TZS 35,000 | USD 28 |
| Regular statement of a/c (Monthly) | Free | Free |
| Interim/additional statement | TZS 1500 per page | USD 1.50 per page |
| Issue of bankers' cheque | TZS 40,000 | USD 30 |
| Cancellation of bankers cheque/DD | TZS 20,000 | USD 15 |
| Issue of Duplicate Bankers cheque/Demand Draft/ Duplicate FDR | TZS 30,000 | USD 20 |
| Application charge for Treasury Bond | TZS 100,000 | USD Equivalent to TZS 100,000 |
| Issue of Balance certificate (Saving Account) | TZS 20,000 | USD Equivalent to TZS 20,000 |
| Issue of Balance certificate (Current Account) | TZS 50,000 | USD Equivalent to TZS 50,000 |
| Signature verification and Photo Attestation charges for Domestic A/c Holders | TZS 10,000 | USD Equivalent to TZS 10,000 |
| Verification of Documents such as KYC Documents along with verification of Photo and Signature of Customer Mentioned account with Bank of India- in India /Overseas | TZS 25,000 | USD Equivalent to TZS 25,000 |
| Savings bank customer Identification card- One time | TZS 20,000 | USD 10 |
| Dormant a/c Activation Per Activation Fees | Individual TZS 5,000 Corporate TZS 12,000 | Individual USD 3 Corporate USD 6 |
| Account Freezing/un freezing Charges | Free | Free |
| SMS Alert facility | Free | Free |
| Email Alert Facility | Free | Free |
| Monthly Statement on Registered Email | Free | Free |
| Balance Inquiry (Over the Counter) | Free | Free |
| Charges for Deletion of Decease Person Name from the Saving Account | Free | Free |
| Charges for Addition/modification Account such as Change in respect of Corporate A/c | TZS 20,000 | USD 10 |
| Updating of Mobile No. in A/c (SB,CD,OD) | Free | Free |
| Change /Modification in Address (SB,CD,OD) | Free | Free |
| Issuance of No Dues Certificate for Non-Borrowers. | TZS 10,000 | USD 7 |
| Ledger Folio Charges per Folio (40 lines per Folio) only for Current and Overdraft Accounts | TZS 6,000 per Folio | USD 4 per Folio |
| Postages/Courier Charges Inland/Foreign | TZS 30,000 or actual charges whichever is higher | USD Equivalent to TZS 30,000 |

**E. CLEARING SERVICES**

| Item | Charge/Fees | |
|---|---|---|
| | TZS A/c | USD A/c |
| Within walking distance-1 km | TZS 70,000 | USD 45 |
| Far off distance –more than 1 km | TZS 95,000 | USD 65 |
| Cheque returned charges –financial reasons (inward/outward) | TZS 70,000 | USD 55 |
| Inward/outward cheque collection -USD | 0.60% Min comm.18 postages 90 | 0.60% Min comm.18 postages 90 |

**CREDIT MATTERS**

| Charge/Fees | | |
|---|---|---|
| **Proposal Processing Charges: -** | | |
| New Overdraft/Term Loan/Demand Loan | 1.50% of sanctioned limit (Regular Limit – 1.50% for 12 Months) | |
| TOD/TOL/ADHOC | Proportionate to 1.50% for TOL/TOD/ADHOC Period minimum USD 60 | |
| New NFB BG/LC Facility | 1.50% of sanctioned limit (Regular Limit – 1.50% for 12 Months) | |
| Review of Overdraft Limit | 1.50% on entire sanctioned amount. | |
| Review of Term Loan Demand Loan Personal Loan Vehicle Loan Loan Against Property Etc. | 0.15% maximum USD 600 or TZS 1.20Mn on the reviewed amount and 1.50% on the additional Term Loan /Demand Loan amount. | |
| Schematic Lending up to 36 months/Staff Loan | Nil | |
| Prepayment charges | 2.50% of the prepaid loan amount. | |
| Documentation charges for New Overdraft Limit/Term Loan/Demand Loan/Non Fund base Limit | Actuals as per advocate Bill + 0.30% handling charges<br>1) No Documents charges would be applicable for TOD/TOL/ADHOC Limit, however actual expenses if any to be recovered.<br>2) Documentation charges also NOT Recoverable for the Loan/Overdraft against FDR. | |
| Charges for Amendments/Modification of Sanction Terms | 0.25% on the sanctioned limit | |
| | **We enumerate the illustrative instances of Modification in Terms and Conditions to be effected at the request of the Borrower where this charge will be levied: -**<br>1) Substitution of Collateral Securities/Personal Guarantee<br>2) Release of Personal Guarantee/Collateral Security.<br>3) Interchangeability of limits.<br>4) Change in project/items of Machinery<br>5) Ceding of charges on assets(Pari-Passu)<br>6) Restructuring, Rephasement of Loans/ Deferment of Loan installments.<br>7) Approvals for mergers & amalgamations.<br>8) Any other miscellaneous credit related approvals. | |
| Revalidation of Sanction | **25% of Applicable PPC Charges on Overdraft Limit/Term Loan/Demand Loan** | |
| Lead bank Charges | **USD 1000 or equivalent in TZS per annum/one time** | |
| Fee for Opening Escrow/TRA A/cs (Trust and Retention A/cs) | **Where**<br>**We are Lead bank: Nil**<br>**We are Not Lead Bank:**<br>USD 500 or equivalent in TZS per annum/one time | |
| Charges for Supplying copies of Loaning Documents to Customer. | First instance: Free<br>**USD 10 or equivalent in TZS for further requirement.** | |
| Non/Delayed Submission of Audited Financial Statements of the Company OR wherever applicable | **USD 100 or equivalent in TZS per month or part thereof**<br>**Note:-**Audited Financial statements of the firm/company within 6 months from closure of Financial Year or as approved by TRA for the relevant year. | |
| Inspection charge | TZS 30,000 per visit/inspection or at least once in quarter whichever is higher. | TZS 50,000 or equivalent to USD per visit /inspection or at least once in quarter whichever is higher. |
| | **Note:-**<br>1) Out of Pocket Expenses to be recovered additionally along with regular inspection charges wherever applicable<br>**2) Project Monitoring Inspection Charges/Technical Due Diligence Inspection charges:** Considering the fact that this inspection is proposed for safeguarding banks Interest, normal inspection charges besides travelling, boarding/lodging expenses are to be recovered from the borrower. | |
| Issuance of No objection certificate (NOC) | **USD 100 or equivalent in TZS** | |
| 1st party/3rd party Overdraft/Loan against deposit of our Bank (BOITL) | Waiver of Processing & Documentation charge. | |
| Overdraft/Term Loan/Demand Loan Conversion Charges (Currency Conversion) | For Overdraft account 0.50% of Sanction Limit.<br>For Term Loan/Demand Loan 0.50% of O/s Amount | |
| Earmarking of Limits | **USD 500 or equivalent in TZS per annum** | |
| Non Compliance of Sanction terms/Commitment charges | **1.00% additional Penal Interest to be charge till compliance of Sanction terms** | |
| **D&B/ Other Credit Information Search for per Borrowal a/c (New/Additional/Review of limit)** | | |
| Up to TZS 20 Mn/USD 10,000 (Only for new and additional Limit. **Review – No charge**) | USD Facility<br>USD 5 | TZS Facility<br>TZS 5,000 |
| Over USD 10,000 to USD 50,000/ Over TZS 20 Mn up to TZS 100 Mn | USD 10 | TZS 20,000 |
| Over USD 50,000/TZS 100 Mn | USD 50 | TZS 100,000 |
| D&B Search for non-Borrower, on request | USD 50 | TZS 100,000 |
| Charges for Furnishing copy of Credit Information report obtained from CIC | **TZS 20,000** | **USD 10** |

| | | |
|---|---|---|
| **Guarantee (Performance/Financial) :-** | | |
| Guarantee Commission | 1.35% per quarter or part thereof minimum for one quarter. | |
| Guarantee against 100% cash margin | 50% concession on the above rate | |
| Swift Charges | **As Applicable** | |
| Postages | **As Applicable** | |
| Revert of Guarantee before Expiry | **Minimum 1 Qtr BG Commission to be recovered for part of quantum of full guarantee commission to be recovered** | |
| Closure of Guarantee After Expiry of Claim Period | Nil | |
| Invoke of Guarantee | **USD 200 or equivalent in TZS** | |
| | **A. Financial Guarantees: -**<br>1. In favour of Customs/Excise/Tax Authorities towards tax/Duties payment Etc.<br>2. Favouring Courts for Release of Amounts.<br>3. For Guaranteeing Loan payments.<br>**B. Performance Guarantees: -** | |
| | 1. In lieu of earnest money deposit<br>2. In lieu of tender deposit<br>3. In lieu of security deposit<br>4. To obtain advance payments (generally exports)<br>5. To obtain mobilization advance (generally domestic)<br>6. Towards Direct/indirect taxes to govt. in respect of specific transaction.<br>7. For Direct/indirect taxes disputes with tax Authorities.<br>8. For payment for supplies/services made /rendered<br>9. For Securing retention amount<br>10. For Bidding/tendering for Project Contacts<br>11. For Performance in terms of any agreed contact.<br>**Note: - No processing charges or documentation charges are to be levied in case of Casual BG limits issued against 100% or more cash margin.** | |
| **Imports :-** | | |
| LC Opening charges | 1.35% per quarter +SWIFT charges USD 30/- | 1.35% per quarter +SWIFT charges USD 75/- |
| Against 100% cash margin | 50% concession on the above rate i.e. 0.67% per quarter +SWIFT charges USD 30/- | 50% concession on the above rate i.e. 0.67% per quarter +SWIFT charges USD 75/- |
| LC Amendment Charges | Per amendment 0.40% of LC amount (minimum USD 60 and Maximum USD 325) +SWIFT charges USD 30 (Same for LC against 100% cash margin) | |
| Acceptance of bills under LC | 0.60% of Bill amount Min USD 30 Maximum USD 180 | |
| Retirement of bills under LC | 0.60% of Bill amount Min USD 30 Maximum USD 360 | |
| Inward Bills for Collection | 0.30% of Bill amount minimum USD 150 | |
| **Exports:-** | | |
| Negotiation of Bills under LC | 0.60% of Bill amount Minimum USD30 Maximum USD 360 | |
| Confirmation of Export LC | 0.90% per quarter +SWIFT charges USD 30/- | |
| LC Advising Charges | USD 150 | |
| Export Bills for Collection | 0.60% of Bill amount Minimum USD 30 Max USD 360. | |
| Charges for Certifying invoices subsequent to negotiation | **USD 10 Per Invoice** | |
| Clean payment Received under LC | **USD 100 per occasion** | |
| Advice of transfer in transferable LC | **USD 100 per advice of transfer and acceptance commission at 0.30% Minimum USD 100** | |

**OTHER DISCLOSURES**
**(VIAMBATANISHI NYINGINEZO)**

| No. | ITEM/TRANSACTION | USD | TSHS |
|---|---|---|---|
| 1.0 | **Base or Prime Lending rate** | 7.50% p.a. | 14.50% p.a. |
| 2.0 | **Maximum Spread above Base or Prime Lending rate** | 7.00% | 7.00% |
| 3.0 | **Penal interest** | | |
| a) | For Non Compliance of Terms of sanction | 3% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| b) | For Overdrawing/ Excess Drawings due to non – payment of interest/ Instalments/ Charges | 5% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| 4.0 | **Deposit Rate** | | |
| i) | Current Deposit | Nil | Nil |
| ii) | Savings Bank Deposit | 0.50% p.a. | 2.50% p.a. |
| iii) | Fixed/Recurring/QIC/MIC deposit | Up to USD 10,000 | Up to TZS 10,000,000 |
| | 6 months | 2.50% | 6.25% |
| | Over 6 months | 3.00% | 7.25% |
| | | Over USD 10,000 | Over TZS 10,000,000 |
| | 6 months | 3.00% | 6.75% |
| | Over 6 months | 3.50% | 7.75% |
| | * No interest is payable in case of premature withdrawal of fixed deposits | | |

**No Penalties & Other sanctions have been imposed by Bank of Tanzania (BOT)during the Period covered by the Disclosure**

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name. | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Antaryami Sarangi | Managing Director | Signed | 03.04.2023 |
| 2. | Heriabdiel Ayoh | General Manager | Signed | 03.04.2023 |
| 3. | Robert Kibona | General Manager | Signed | 03.04.2023 |

217356001

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Sheria iongezewe meno wahusika vitendo ukatili

**KWA** muda mrefu kumekuwa na taarifa mbalimbali kwenye vyombo vya habari kuhusu vitendo vya ukatili wanavyofanyiwa wanawake na watoto katika maeneo mbalimbali, vingi vikiripotiwa kufanywa na watu wa karibu wakiwamo wazazi na walezi.

Miongoni mwa vitendo hivyo ni ubakaji, unajisi na ulawiti dhidi ya watoto wadogo ambao wamekuwa wakifanyiwa kwa asilimia kubwa na watu wa ndani mwao, kwa maana ya wanafamilia. Kwa mujibu wa takwimu za hivi karibuni, vitendo hivyo, kwa asilimia 60 vinafanywa ama na baba, kaka, baba mdogo au mjomba ambao wanaishi pamoja na watoto wanaoathirika na matukio hayo.

Pamoja na vitendo hivyo, kumekuwapo taarifa za wazazi au walezi kuwafanyia ukatili kwa njia ya vipigo na kuwaumiza sehemu za viungo kama vile mikono, vidole na hata sehemu za siri kwa madai ya kudokoa mboga au kuiba fedha nyumbani au kwa majirani. Vitendo hivyo vimekuwa vikisababisha watoto kupata ulemavu wa kudumu pamoja na kuathirika kisaikolojia.

Mfano halisi ni tukio lililotokea wiki iliyopita katika kijiji cha Nyarugusu mkoani Geita cha mtu aliyefahamika kwa jina la Mathias Daudi, anayedaiwa kumchoma mtoto wake kwa maji ya moto kwa kuingiza mikono yake kwenye sufuria ya maji iliyokuwa jikoni ikichemka kwa madai ya kuiba Sh. 5,000 kwa jirani.

Mtoto huyo ambaye ni mwanafunzi wa darasa la nne, mwenye umri wa miaka 10, anadaiwa kuwa alimpelekea baba yake huyo fedha hiyo aliyodai kuwa ameiokota na hatimaye kuipangia matumizi kisha akatumwa kwenda kununua vitu.

Wakati hayo yakiendelea, mtoto aliporudi alimkuta jirani ambaye alidai kuwa ameibiwa fedha hiyo ndipo baba mzazi alipoamua kumtembezea mwanawe kipigo kabla ya kumchoma kwa maji ya moto.

Mtu huyo tayari ameshatiwa mbaroni kusubiri sheria ichukue mkondo wake kutokana na kitendo hicho baada ya idara ya maendeleo ya jamii kwa kushirikiana na wasaidizi wa sheria kumfuatilia na hatimaye kumkamata.

Pamoja na kutiwa mbaroni, wanasheria hao na maendeleo ya jamii wameweka bayana kwamba mtoto huyo hata akipona, hawezi kurudishwa kwa baba yake kwa kuwa tayari ameathirika kisaikolojia.

Kwa jumla, matukio na vitendo vya ukatili kama hivyo vimekuwa kama dondandugu katika jamii kwa sababu mbalimbali zikiwamo za kiuchumi kwa maana ya umaskini unaozikabili familia nyingi. Katika mtazamo wa haraka mtoto kuumizwa kwa madai ya kuiba Sh. 5,000 au kudokoa mboga jikoni, moja kwa moja ni umaskini wa kipato na wa hali ndani ya familia.

Kwa mantiki hiyo, jitihada zinatakiwa kuzikomboa familia hizi kwa kuziwezesha kupitia ngazi mbalimbali kama mpango wa kunusuru kaya maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Ni imani kwamba kwa kufanya hivyo, familia za aina hiyo zinaweza kwa kiasi kikubwa kujikomboa katika lindi la umaskini.

Pamoja na hayo, sheria zinatakiwa kupewa meno zaidi dhidi ya watu wanaojihusisha na vitendo hivyo kwa sababu watoto kuumizwa viungo au kufanyiwa ukatili kama ubakaji na ulawiti, vinasababisha madhara ya kisaikolojia na kimaumbile ambayo si rahisi kutoka katika akili zao.

Kwa maana hiyo, ni vyema sheria zilizopo kama vile adhabu ya kifungo cha maisha au miaka 30 jela, kutazamwa upya ili kuwanusuru watoto ambao ni tegemeo kwa maendeleo ya taifa na kizazi kijacho.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

## Mgogoro TLP unaoendelea unakosa hata chembe ya faida

**NI** uchaguzi ulioahirishwa ghafla, huku wajumbe wa mkutano mkuu kutoka mikoa mbalimbali wakiwa wamefika jijini Dar es Salaam, kwenye uchaguzi wa mwenyekiti mpya wa kurithi nafasi iliyoachwa na Augustine Mrema.

Lawama za kuahirishwa kwa uchaguzi huo, sasa inaelekezwa kwa kiongozi katika nafasi ya juu ya utendaji ndani ya TLP, ambaye inadaiwa na baadhi ya wajumbe na wagombea wa nafasi hiyo, kuwa alijitwisha madaraka na kutangaza kuahirishwa uchaguzi huo.

Sababu za kuahirishwa zikidaiwa kuwa haukuwepo usalama, lakini wagombea wanapinga na kueleza kuwa kuna kiongozi mwandamizi mtendaji, naye alikuwa mmoja wa wagombea wa nafasi hiyo na alipobaini hawezi kushinda, akavuruga.

Tayari wagombea wamefikisha malalamiko katika Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na inadaiwa kuna hatua zinazochukuliwa, katika ofisi ya TLP.

Sasa kama hali ndiyo hiyo, najiuliza huo mgogoro wa TLP ni kwa faida ya nani? Nani yuko nyuma yake, kwa maoni yangu nahisi mgogogro unasababisha chama kuendelea kuyumba kwa mgogoro na kushindwa kuaminika kwa wananchi?

Ninadhani, ipo haja kwa viongozi wa TLP kuangalia upya mikakati itakayosaidia kukifufua chama hicho, ambacho kwa muda mrefu kimekuwa kikisuasua kutokana na kupitia migogoro mbalimbali ya uongozi isiyoisha.

Mara tu baada ya kumaliza msiba wa Mwenyekiti Mrema, uongozi wa TLP uliwatangazia wanachama wake wa zamani walioondoka kutokana na sababu mbalimbali, zikiwamo za kiuongozi, sasa warejee wakijenge chama chao.

Hata hivyo, ushuhuda wangu kilichotokea Machi 6 mwaka huu, ni wazi chama hicho bado hakijatulia, hivyo ninadhani ipo haja kwa viongozi kukaa na kuangalia uwezekano wa kuwekana sawa, ili kazi iendelee.

> **Ingependeza kama viongozi wangetafakari na kubaini mahali walikopishana na kuwa chanzo cha migawanyiko ya sasa, inayosababisha baadhi kukimbilia kwa Msajili wa Vyama vya Siasa, kutafuta muafaka.**

Ikumbukwe kwamba, hatua ya kupelekana kwa Msajili wa Vyama vya Siasa, maana yake chama kimeshindwa kumaliza migogoro ya ndani, hali inayoweza kusababisha kuendelea mvutano usioisha.

Ingependeza kama viongozi wangetafakari na kubaini mahali walikopishana na kuwa chanzo cha migawanyiko ya sasa, inayosababisha baadhi kukimbilia kwa Msajili wa Vyama vya Siasa, kutafuta muafaka.

Pia wanachama na viongozi hao, wakumbuke kuwa migogoro ndani ya vyama inaua demokrasia na inaviua vyama vyenyewe, iwapo viongozi wake hawatakuwa makini, kwani mifano ipo mingi kwa vyama vilivyokumbwa na migogoro aina hiyo.

Miongoni mwake ni TLP yenyewe ambayo kwa muda mrefu imekuwa na migogoro iliyosababisha ikose madiwani na wabunge na ikitupa jicho nje, kuna vyama kadhaa ambavyo vimekwama kuendesha siasa.

Vyama hivyo tajwa vya mfano vipo, lakini havina nguvu kama zamani, hasa baada ya kukumbwa na migogoro ya kiuongozi ambayo kimsingi, ni wazi haiwezi kuwa na manufaa yoyote kwa vyama vya siasa, zaidi ya kuviua.

Mazingira ambayo TLP imepitia, yangefaa kuwa shule ya kuwafanya viongozi wake kujifunza kitu na kujipanga upya na kuondokana na migogoro ambayo imechangia kuifanya ikimbiwe na wanachama wengi.

Historia za migogoro ndani ya vyama vya upinzani, haijawahi kuviacha salama zaidi ya kuvisambaratisha, hivyo ninadhani ipo haja kwa TLP kukaa na kutafakari ni wapi viongozi wanapeleka chama hicho na kuchukua hatua sahihi za kukisimamisha upya chama hicho kama ambavyo waliahidi baada ya kumaliza msiba wa mwenyekiti wao wa zamani.

## HABARI KITAIFA

# Darasa la saba wakumbukwa ufadhili

**Na Restuta James**

SERIKALI imewakumbuka wahitimu wa 'darasa la saba' kwa kufadhili mafunzo ya ujuzi kwenye fani za uchomeleaji, ufundi bomba wa viwandani na majumbani.

Ufadhili huo unawalenga vijana wenye miaka 15 hadi 35 ambao wako tayari kujiunga na fani hizo, zitakazotolewa katika vyuo vinne vya Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA).

Taarifa ya VETA iliyotolewa kwa umma jijini Dar es Salaam jana, ilieleza kuwa mafunzo hayo yanalenga kukuza ujuzi katika fani hizo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, vyuo vilivyochaguliwa kutoa mafunzo katika awamu ya tatu ya ufadhili huo VETA Gorowa, Dodoma, Lindi na Manyara na kwamba vijana watakaochaguliwa kujiunga na mafunzo hayo watafundishwa kwa nadharia na vitendo, darasani na viwandani.

"Katika mwaka huu wa fedha ofisi imepanga kutoa mafunzo ya ujuzi katika fani za uchomeleaji vyuma viwandani, ufundi bomba wa viwandani na ufundi bomba wa majumbani...mafunzo yatatolewa kwa mfumo wa uanagenzi vyuoni na viwandani, ambapo baada ya mafunzo ya nadharia na vitendo vyuoni, wanafunzi watakaofuzu watapata fursa ya kufanya mafunzo ya vitendo viwandani chini ya uangalizi wa ATE na GOPA," ilieleza taarifa hiyo na kuongeza kuwa wanafunzi watakachaguliwa watalipiwa gharama zote za mafunzo.

Taarifa ilitaja vigezo vya kujiunga na mafunzo hayo kuwa mwombaji awe raia wa Tanzania, mwenye umri wa 15 hadi 35, pamoja na idhini ya maandishi ya mlezi au mzazi kwa vijana wenye umri chini ya miaka 18.

Mafunzo hayo yanatolewa chini ya mradi wa kukuza ajira na ujuzi kwa maendeleo ya Afrika (E4D) na kufadhiliwa na Wizara ya Ujerumani ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (BMZ), Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo la Norway (NORAD), Umoja wa Ulaya (EU) na Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo la Korea ya Kusini (KOICA).

Aidha, ufadhili huo unaratibiwa kwa ushirikiano kati ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu, VETA na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ).

Vijana wanaotaka kujiunga na mafunzo hayo wamepewa siku 13 za kuwasilisha maombi yao kuanzia Jumamosi iliyopita hadi Alhamisi wiki ijayo; na mafunzo yanatarajiwa kuanza Aprili 17, mwaka huu.

**Katika mwaka huu wa fedha ofisi imepanga kutoa mafunzo ya ujuzi katika fani za uchomeleaji vyuma viwandani, ufundi bomba wa viwandani na ufundi bomba wa majumbani...**



Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya EFTA Tanzania, Nicomed Bohay akifafanua jambo kuhusu matumizi ya mashine za kampuni ya New Holland katika kilimo na elimu juu ya fedha, wakati wa mafunzo kwa wakulima wa wilaya za Dodoma, yaliyoandaliwa na taasisi hiyo kwa kushirikiana na kampuni ya Hughes Agriculture Tanzania jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Simbachawene asisitiza dhamira utumishi bora

**Na James Mwanamyoto,**

DODOMA

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene ameeleza dhamira yake ya kushirikiana na watumishi wa ofisi yake katika kutekeleza jukumu la kuwasimamia watumishi wa umma kuwahudumia wananchi badala ya kufanya mambo ambayo yanakwamisha azma hiyo.

Simbachawene ameweka wazi dhamira hiyo ya kuwasimamia watumishi wa umma kutekeleza wajibu wao kikamilifu pindi alipowasili ofisini kwake na kuzungumza na watumishi wa ofisi yake baada ya kuapishwa na Rais Samia Suluhu Hassan Aprili 2, mwaka huu, Ikulu jijini Dar es Salaam,

Alisema rasilimali watu ni muhimu sana katika maendeleo ya taifa lolote, hivyo ni lazima watumishi wa umma wafanye kazi kwa mujibu wa kanuni, sheria, taratibu, miongozo na Katiba ya Tanzania ambayo ndiyo sheria mama.

Waziri alisema wateja wanaofuata huduma katika taasisi za umma wamekuwa wakilalamika kutopatiwa huduma nzuri na kwa wakati na kuongeza kuwa baadhi ya watumishi wamekuwa wakifanya shughuli binafsi mahali pa kazi wakati wananchi wakisubiri kupatiwa huduma.

"Muda ambao mtumishi wa umma anatakiwa kufanya kazi ni saa nane, lakini utakuta mtumishi akiingia kazini anakuwa na pilika nyingine ambazo si za kazi anayopaswa kuifanya. Mfano muuguzi au mwalimu anaposhindwa kuwajibika, madhara yake ni makubwa. Taifa linapata hasara kubwa kwa sababu rasilimali watu haitumiki ipasavyo," alisisitiza.

Aliongeza kuwa mtumishi anaingia kazini na simu ambayo ina makundi mengi, akianza kuwasiliana na makundi matatu tu saa moja ya kazi imeondoka na kwa kuwa ana makundi ya majirani, vikoba na mengineyo, hivyo akiendelea kushiriki kinachojadiliwa, matumizi ya simu yanachukua muda mwingi wa kazi na kusababisha wananchi kutopatiwa huduma wanayostahili.

"Niwaombe watumishi wenzangu na wataalam wangu tushirikiane na tuwe wazi ili tupate mwelekeo sahihi wa namna ya kurekebisha hii changamoto ya watumishi wa umma kutumia muda wa kazi vibaya badala ya kuwahudumia wananchi ambao kodi zao ndio zinatulipa mishahara," alisema.

Simbachawene alifafanua kuwa serikali imewekeza rasilimali fedha kwa mtumishi wa umma ili kutoa huduma kwa wananchi katika saa nane zote za kazi, hivyo ofisi yake ina wajibu wa kutafuta suluhisho la nini kifanyike kuhakikisha watumishi wa umma nchini wanatekeleza wajibu wao ipasavyo.

Alisema katika nchi zingine hawaruhusiwi kutumia simu muda wa kazi ili kutoa huduma iliyokusudiwa na kuongeza kuwa waajiri wameweka utaratibu mzuri wa kuzihifadhi simu za watumishi pindi wanapoingia kazini na kuwapatia kwa ajili ya kuwasiliana na ndugu na jamaa zao wakati wa chakula cha mchana na wanapotoka kazini.

Waziri Simbachawene aliwashukuru watumishi wa ofisi yake kwa kumpokea vizuri na kuendelea kuomba ushirikiano wa kiutendaji ili kumsaidia Rais Samia kutimiza azma yake ya kuhakikisha watumishi wa umma wanafanya kazi kwa uadilifu, kuwajibika kwa wananchi na kuwa na tija katika maendeleo ya taifa.

## KABWELA

**Na Fadhil Mohammed**



# Mahakama yabariki aliyemuua mtoto wa kaka yake auwawe

Na Kulwa Mzee

MAHAKAMA ya Rufani, imebariki Vitalis Kambilanga kunyongwa hadi kufa kwa kosa la kumuua kwa kukusudia mtoto wa kaka yake, Kipawa Kambilanga (7).

Uamuzi huo ulitolewa hivi karibuni mbele ya jopo la majaji watatu, Gerald Ndika, Ignas Kitusi na Lilian Mashaka baada ya kupitia rufani ya Vitalis na kuitupa baada ya kuona haina mashiko.

Katika rufani hiyo, Kambilanga alikuwa akipinga hatia na adhabu aliyopewa katika Mahakama Kuu, Kanda ya Morogoro.

Jopo katika uamuzi wake lilipoketi Dar es Salaam, lilisema kulingana na ushahidi uliotolewa, hakuna shaka kwamba mrufani alimuua Kipawa.

Katika hukumu hiyo, jopo lilisema hakimu wa mahakama ya chini alimhukumu kwa usahihi mrufani na kumpa adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Kutokana na hali hiyo lilisema mahakama iliamua tupilia mbali rufani yake.

Katika shauri hilo, ilidaiwa kwamba mrufani alitenda kosa hilo Julai Mosi, 2016, saa 10:00 jioni katika kijiji cha Tanganyika Masagati, Kilombero mkoani Morogoro.

Ilidaiwa kuwa siku ya tukio, kaka mkubwa wa mrufani, Norbert Kambilanga, alirejea nyumbani kwake kijijini hapo na hakumkuta mtoto wake wa kiume, Kipawa na baadaye Jantalina Kambilanga alimweleza kuwa ameenda Mto Rufiji akiwa na mrufani.

Ilidaiwa kwamba mpaka usiku mtoto huyo hakuwa amerudi ndipo Norbert akiwa na watu wengine walienda mtoni kumtafuta bila mafanikio.

"Siku iliyofuata asubuhi utafutaji uliendelea ambapo kando ya mto waliona suruali ya jeans, tochi na ndala za mrufani na mbele yake waliona mwili wa Kapawa chini ukiwa na jeraha kichwani.

Kambilanga alitoa taarifa kwa uongozi wa kijiji siku hiyo hiyo na kubainika kwamba mrufani na mwanawe wa kambo, Erenensia Kambilanga, hawakuwapo kijijini hapo huku mkewe Rustica Njewike, akipatikana akiwa amejeruhiwa.

Taarifa ya tukio hilo ilitolewa polisi na mrufani alikamatwa kijiji cha Ipinde na aliwapeleka askari na wanakijiji wengine eneo la tukio.

Ilidaiwa kuwa mrufani alikiri kutenda kosa hilo. Mrufani pia aliwapeleka watu hao eneo lingine umbali wa kilometa 10 na kwamba walimkuta mwanawe wa kambo Erenensia, amelala chini akiwa amepoteza fahamu.

Katika utetezi wake, mrufani alikana kutenda tukio hilo huku nae akikiri kuwa na mgogoro na mkewe Rustica huku akimtuhumu kaka yake Kambilanga kumsaliti.




Ofisa Mauzo wa kampuni ya Bia ya Serengeti, Emila Machuve (kulia), akizungumza kwa njia ya mtandao na mshindi wa gari aina ya IST, Shamimu Hemedi Mushi wakati wa droo ya mwisho ya promosheni ya ya bia ya Pilsner Lager ya "Kapu la Wana" jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mwakililishi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania, Salim Mgufi. Makabidhiano ya gari hilo, yatafanyika jijini Arusha mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wachimbaji wadogo 700 kujadili changamozo zao

Na Beatrice Shayo

ZAIDI ya wachimbaji wadogo wa madini 700 na wadau wa sekta hiyo, wanatarajia kukutana leo kujadili changamoto zinazowakabili, ikiwamo viwanda kuagiza kwa wingi malighafi kutoka nje ya nchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), Dk. Venance Mwasse, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na mkutano huo wa siku mbili ambao utafanyika jijini Dar es Salaam. Alisema moja ya changamoto zitakazojadiliwa ni viwanda vingi kuagiza malighafi nje ya nchi ingawa zinapatikana nchini, hivyo wanataka kujua tatizo lipo wapi ipatikane suluhu.

Mwasse alisema wanakutana na wachimbaji wadogo, wachimbaji wa madini ya viwandani na wenye viwanda ambao wanatumia madini hayo na kujadiliana masuala mbalimbali.

Alisema lengo la kuwakutanisha wadau hao ni kujua changamoto ambazo zinawakabili na nini kinachosababisha viwanda vinatumia malighafi kutoka nje ya nchi na sio za Tanzania.

Aidha, alisema licha ya wadau hao pia wamewaita wengine kama Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Tume ya madini na watoaji wa leseni, ili kama viwanda vinachangamoto ya ubora watoe suluhisho.

Alisema kutakuwa na wataalamu wa madini ambao wanajua madini yanapopatikana huko ardhini wenye ramani ya upatikanaji wa majini, hivyo watatoa elimu ili mchimbaji kumpa uhakika mwenye kiwanda anavyompelekea madini.

Alisema lengo la mkutano huo ni kuhakikisha kila mmoja ananufaika kupitia sekta ya madini ili kufikia ajenda ya viwanda kupitia madini kwa kuchangia asilimia 10 katika pato la taifa ifikapo 2025.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI), Leodegar Tenga, alisema nchi inataka kujenga uchumi wa viwanda hivyo kinachofanyika ni muendelezo wa kufikia malengo yaliyopangwa.

# TAFORI yaagizwa kufanya utafiti kudhibiti uharibifu

Na Idda Mushi, MOROGORO

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, ameitaka Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) kufanya utafiti ili kudhibiti uharibifu wa misitu, kuboresha sheria zinazosimamia taasisi hiyo na kuongeza mapato yatokanayo na kuuzwa kwa mazao ya misitu nje ya nchi.

Mchengerwa aliyasema hayo jana mjini hapa wakati wa uzinduzi wa bodi ya 12 ya TAFORI na kuitaka bodi hiyo kuja na mkakati wa kuongeza mapato yatokanayo na mazao ya misitu na nyuki ikiwemo asali kwa kutoa elimu kwa wananchi na wawekezaji ili kukuza sekta hiyo.

Alisema serikali inaamini kuwa bodi hiyo pia itawapatia ushauri wa kitaalamu kusaidia taasisi hiyo na wizara kwa ujumla, ikiwemo marekebisho ya sheria kulingana na mahitaji yaliyopo na zitakazosaidia kuunganisha au kupangua baadhi ya majukumu au taasisi kulingana na mazingira na mahitaji.

"TAFORI ifanye utafiti ili kuongeza mapato sekta ya misitu na nyuki kutoka takribani Sh. bil. 250 ya mwaka jana (2022) kuongeza zaidi kwa miaka inayokuja. Nataka kuona ndani ya muda mfupi tunapata fedha nyingi zaidi kutokana na soko la kimataifa na soko la ndani, hatuwezi kufikia huko kama hatujatoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa mazao ya nyuki," alisema.

Alisema licha ya TFS kuwa na mashamba ya miti 24 yenye ukubwa wa zaidi ya hekta laki tano, hifadhi za nyuki 12 pamoja na manzuki 204 bado uzalishaji wa mazao yatokanayo na nyuki ni kidogo na hayaridhishi.

Mchengerwa akaagiza sekta ya misitu na ufugaji nyuki kujiimarisha kwa kuongeza uzalishaji wa mazao ya misitu na nyuki husani magogo, asali na nta kwa kuwa wamedhamiria kujielekeza katika uchumi wa kipato cha kati ifikapo 2025.

Katibu Mkuu wa Maliasili na Utalii, Dk. Hassan Abbas, alisema sekta ya maliasili ina mchango mkubwa kiuchumi kwa kuchangia asilimia 3.3 kwenye pato la taifa.

Awali, Mwenyekiti wa bodi ya TAFORI, Prof. Verdiana-Grace Masanja, aliahidi bodi hiyo kufanyia kazi maelekezo yaliyotolewa na kuhimiza umuhimu wa serikali kuwekeza zaidi kwenye shughuli za utafiti, ili kufanikisha malengo mbalimbali yanayowekwa kuinua sekta hiyo.

Wajumbe wengine wa bodi hiyo ya TAFORI ni Prof. Dos Santos Silayo ambaye ni Makamu Mwenyekiti, Katibu Dk. Revicatus Mushimbusi, Prof. Faustine Kamuzora, Dk. Zanifa Limba, CPA Beatrice Lipu, Dk. Hulda Mpunjo, John Nchimbi, Xavier Ndalahwa na Daniel Pancras.



# Mradi kuokoa wananchi kutumia maji yasiyo salama yenye madini

**Na Allan Isack,** ARUMERU

WANANCHI wa Kijiji cha Engutukoit katika Kata ya Oldonyowas, Halmashauri ya Arusha, wilayani Arumeru, wataondokana na adha ya kutumia maji yenye kiwango kikubwa cha ongezeko la madini ya fluoride baada ya Shirika la Climate Change Solution (CCS) kuanzisha mradi wa kuchuja maji.

Shirika hilo lisilo la kiserikali, limejipanga kuanza kutekeleza mradi huo ili kuondoa kiwango cha madini ya fluoride kwa matumizi ya wananchi wa kijiji hicho.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na mashirika mbalimbali, maji ya eneo hilo yana madini ya fluoride yaliyozidi miligramu 24 kwa lita moja ya maji ambayo yana madhara kwa matumizi ya binadamu.

Akiwasilisha jana mpango wa utekelezaji wa mradi huo kwa wajumbe wa kikao cha menejimenti ya ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Arusha, Mratibu wa Mradi huo, Jorg Lenkel, alisema shirika hilo linatarajia kutekeleza mradi huo kwa thamani ya Sh. milioni 71.

Mratibu huyo alisema mradi utahusisha ukarabati wa miundombinu ya maji iliyoko kijijini hapo, ujenzi wa tangi lenye ujazo wa lita 5,000 litakalosimikwa mtambo wa kuchujia maji kupitia madini ya mkaa, sambamba na kuongeza vituo vya kuchotea maji.

Lenkel alisema lengo la kutekelezwa kwa mradi huo ni kuweka mfumo utakaowezesha upatikanaji wa maji safi na salama kwa ajili ya matumizi ya nyumbani kwa wakazi wa eneo hilo kutokana na kukabiliwa na tatizo la kutumia maji yenye fluoride ambayo yana madhara kwa binadamu.

Pia alisema mradi huo utatekelezwa kwa kipindi cha miezi miwili kuanzia sasa na unatarajiwa kuwahudumia wananchi wote wa kijiji cha Engutukoit.

Halmashauri imeupokea kwa mikono miwili mradi huo kutokana na kutambua kuwa wananchi wa maeneo hayo wanatumia maji yenye madini fluoride ambayo yamesababisha madhara kwa wananchi wakiwamo watoto kupinda miguu, kuzaliwa wakiwa na vichwa vikubwa na kuoza meno kuwa na rangi ya kahawia.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Arusha, Omary Sembe, aliwataka wadau hao kutekeleza mradi kwa kuzingatia viwango vya ubora unaoendana na thamani ya fedha.

Pia aliwataka wadau hao kuzingatia kanuni,sheria na utaratibu wa nchi ikiwamo mila na desturi za wakazi wa eneo hilo.

Awali, CCS ilikuwa linafanya kazi kwa kushirikiana na shirika la Oikos East Africa kutekeleza mradi kwa kushirikiana na Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Arumeru kwa ufadhili wa Free State of Saxony kupitia Foundation North South Bridges, The Working Group wa Ujerumani.

# Wapongeza kuanzishwa dawati ulinzi watoto

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WADAU wa kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa watoto, wamepongeza hatua ya Shirika la So They Can (STC) ya kuanzisha madawati ya ulinzi na usalama wa mtoto shuleni huku wakisema ni hatua nzuri ambayo itawasaidia wanafunzi kutoa taarifa za ukatili wanaofanyiwa.

Wadau hao walitoa pongezi hizo jana kuhusu jitihada zilizofanywa na STC wakati yakihitimishwa mafunzo ya siku tatu yaliyoandaliwa na shirika hilo kwa lengo la kutoa elimu ya kuanzishwa madawati hayo kwa walimu, wazee wa mila, watoa ushauri nasaha, mabalozi wa kuteta na watoto na viongozi wa wilaya na kata nne za Halmashauri ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara.

Akizungumzia uanzishwaji wa madawati hayo, Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, Mathias Focus, alisema elimu iliyotolewa itasaidia kuongeza kasi ya kutoa taarifa za ukatili wanaofanyiwa watoto.

**Asilimia kubwa watoto wanaofanyiwa ukatili ni kuanzia miaka mitatu mpaka 18 pia wako wanaobakwa, kunajisiwa na kuketwa.**

Pia alisema awali hali ilikuwa mbaya na chanzo cha ukatili huo unasababishwa na wazee wa kimila kumalizana kienyeji kwa kupeana kondoo na ng'ombe, hivyo husababisha kuongezeka kwa matukio hayo.

"Asilimia kubwa watoto wanaofanyiwa ukatili ni kuanzia miaka mitatu mpaka 18 pia wako wanaobakwa,kunajisiwa na kukeketwa," alisema Focus.

Ofisa huyo alisema Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 inaelekeza kwamba mtu yeyote anayeshuhudia mtoto akifanyiwa ukatili, anatakiwa kuwajibika kwa kusimama mahakamani na kutoa ushahidi ili haki itendeke na haijalishi kama ni mama, baba au jirani.

Focus alisema wazee wa kimila wanaosaidia kumaliza kienyeji kesi za ukatili huo wanapaswa kufungwa miezi mitano au kulipa faini Sh. milioni moja.

Mkuu wa Dawati la Jinsia kutoka Jeshi la Polisi mkoani Manyara, Mkaguzi Msaidizi Wilness Kimario, alisema asilimia 60 ya ukatili wanaofanyiwa watoto hao unafanyika nyumbani kwao na asilimia 40 wanafanyiwa wakiwa shuleni.

Kimario alisema kwa elimu iliyotolewa na shirika hilo itasaidia kwenye kesi za ukatili kuripotiwa na kufanyiwa kazi ili haki itendeke.

Mmoja wa mabalozi kutoka Kijiji cha Ayamango, Peter Abel, alisema elimu hiyo itamsaidia kujua masuala ya kisheria na wapi pa kuripoti vitendo vya ukatili.

Alisema kwa kiwango kikubwa ukatili wanafanyiwa watoto wa kike kuanzia miaka mitatu kwa kubakwa na kuozeshwa na watoto wa kiume kunajisiwa wakiwa na umri kuanzia miaka mitatu.

Meneja Mkazi wa STC, Roselyne Mariki, alisema baada ya kutoa elimu hiyo,wanatarajia kuwapo kwa mabadiliko,pia wanaamini utekelezaji utafanyika kwa viwango vya juu shuleni na nyumbani.




Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo na Mbunge wa Muheza, Hamisi Mwinjuma 'Mwana FA' (wapili kulia), akikabidhi msaada wa vitabu vya misahafu 200 kwa waumini wa dini ya kiislam, wilayani Muheza, mkoani Tanga juzi, wakati wa kongamano la kuelimisha na kukataza mambo yasiyoendana na maadili. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mvua yakwamisha usafiri kwa saa tatu

**Na Mary Mosha,** SIHA

WASAFIRI wanaotumia barabara kuu ya Moshi - Arusha wamekwama zaidi ya saa tatu katika eneo la kwa Msomali, wilayani Siha mkoani Kilimanjaro, baada ya maji kujaa katika daraja lililopo eneo hilo.

Kujaa kwa maji katika barabara hiyo kumetokana na mvua kubwa iliyonyesha usiku wa kuamkia juzi katika maeneo mbalimbali wilayani hapa.

Wakizungumza na Nipashe juzi kwa nyakati tofauti, baadhi ya wasafiri akiwamo Rashid Sudi, aliyekuwa akisafiri kutoka Moshi kwenda Dodoma, alisema kuna haja kwa serikali kuangalia uwezekano wa kutatua tatizo hilo, wa haraka kwa kuwa limekuwa likitokea mara kwa mara katika eneo hilo ambalo ni korofi.

"Kila mara mvua zinaponyesha maji hujaa katika eneo hili,hasa kwenye daraja na kusababisha mafuriko katika maeneo yaliyokaribu nayo," alisema Mwanaisha Juma aliyekuwa akisafiri kwenda mkoani Singida.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Simon Maigwa, alithibitisha kutokea kwa tatizo hilo na alisema mafuriko hayo yalikuwa mengi na kuzuia magari kushindwa kuendelea na safari.

Alisema maji hayo yalijaa kuanzia saa 3:00 asubuhi mpaka 6:00 mchana na walitoa ushirikiano kwa wasafiri ili kuzuia madhara yoyote kutokea kisha kuruhusu magari kuendelea na safari zao.



HABARI KANDA ZIWA

# Serikali yapiga 'stop' adhabu kali shuleni

**Na Vitus Audax,** MWANZA

KAMISHNA wa Elimu nchini, Dk. Lyabwene Mtahabwa, amewaonya walimu wanaoendekeza vitendo vya kikatili kwa wanafunzi zikiwamo adhabu kali ambazo zimekuwa zikiwaathiri kisaikolojia na pengine kusababisha vifo.

Amewataka walimu wenye tabia hizo kuacha mara moja ili kuzifanya shule kuwa sehemu rafiki kwa wanafunzi.

Dk. Mtahabwa alisema hayo juzi, wakati wa ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa Maofisa Elimu wa Mikoa na Halmashauri (REDEOA) unaofanyika kitaifa mkoani Mwanza huku akiwataka walimu kujenga urafiki na wanafunzi ili kuinua kiwango cha ufaulu nchini.

Pia aliwaagiza maofisa elimu hao kuwafikishia ujumbe walimu sambamba na kusimamia hilo kwa kuhakikisha wanaacha ukatili kwa watoto kwa kuacha kuwapiga kama wanyama bali wawalinde na kuhakikisha wanapata elimu bora kama ilivyo dhamira ya serikali.

**Tutawahimiza watumie ujuzi waliofundishwa katika taaluma zao kuhakikisha watoto wanaelewa na sio kumpatia adhabu kali mwanafunzi na kumfanya aogope kwenda shuleni wakati mwingine.**

"Sifa kuu ya mwalimu bora ni upendo si ukatili wanaouendekeza siku hizi. Kuweni na upendo huku mkizingatia kuwa rasilimali ya watoto haiwezi kulinganishwa na rasilimali yoyote hapa nchini," alisema.

Katika hatua nyingine, Dk. Mtahabwa aliwataka walimu kujenga uhusiano mzuri na jamii kwa lengo la kudhibiti vitendo vya ukatili kwa watoto vinavyoelezwa kufanyika katika jamii kwa asilimia 60 huku shuleni vikidaiwa kuwa asilimia 40.

Awali, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Sekta ya Elimu, Dk. Charles Msonde, aliwataka maofisa elimu mikoa na halmashauri kuboresha utendaji kazi ili kuongeza ufaulu kwa wanafunzi.

Alisema wamekuwa wakishuhudia idadi kubwa ya wanafunzi wakishindwa kuendelea na darasa la tano kutokana na kutokujua kusoma, kuandika na kuhesabu hali ambayo haitakiwi kuvumiliwa.

"Nendeni mkalishughulikie hili ikiwa ni pamoja na kuhakikisha mpango wa kuboresha elimu unafika katika maeneo yenu hususani kuhimiza somo la kiingereza kuanzia darasa la tatu ili mwanafunzi akianza kidato cha kwanza awe na uwezo wa kumudu lugha hiyo," alisema Dk. Msonde.

Germana Mung'aho, ni Ofisa Elimu Mkoa wa Morogoro, alisema wako tayari kwenda kwa walimu kuwahimiza kuweka urafiki baina yao na wanafunzi pamoja na wazazi ili kufanya elimu kuwa sehemu rafiki kwa wanafunzi wao.

"Tutawahimiza watumie ujuzi waliofundishwa katika taaluma zao kuhakikisha watoto wanaelewa na sio kumpatia adhabu kali mwanafunzi na kumfanya aogope kwenda shuleni wakati mwingine," alisema Mung'aho.

Mkutano huo unaendelea jijini Mwanza kwa siku nne ukiwa na lengo la kujadili maendeleo ya elimu, fursa na namna ya kukabiliana na changamoto zinazoikabili sekta hiyo ukiwa na kaulimbiu ya 'Uboreshaji wa Miundombinu ya Elimu Unaimarisha Ufundishaji, Ujifunzaji na Ustawi wa Walimu na Wanafunzi.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Musoma vijijini, Denis Ikwabe (kulia mwenye kofia), alipotembelea waathirika wa mafuriko katika kijiji cha Kusenyi, mkoani Mara jana. **PICHA: MATHIAS MARWA**

# Serikali yaombwa kusimamia jenzi wa stendi Kagera

**Na Titus Mwombeki,** BUKOBA

BAADHI ya wananchi mkoani Kagera wameiomba serikali kusimamia kikamilifu ujenzi wa kituo cha mabasi cha Bukoba ili kikamilike mapema na kuondoa adha wanayoipata katika kituo kilichopo kwa sasa.

Inaelezwa kituo cha mabasi kilichopo kwa sasa kinakabiliwa na tatizo la kujaa maji sambamba na wingi wa tope hususani katika kipindi cha mvua. Pia hakuna jengo la abiria kwa ajili ya kujihifadhi pindi wanapofika kituoni hapo.

Wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti, wananchi hao walisema ujenzi wa kituo kipya cha mabasi bado unasuasua tangu ulipoanza mwaka wa fedha 2012/13 na mpaka sasa ni zaidi ya miaka 10.

Jesca Mtashaga, mkazi wa Manispaa ya Bukoba, aliiambia Nipashe kuwa kituo kinachotumika kwa sasa kina matatizo yakiwamo matope kujaa, kutokuwa na jengo la abiria ambao hufika na mabasi ya usiku na kukosa mahali pa kupumzikia.

"Kituo hiki vilevile hakina uzio hali inayohatarisha usalama wa abiria wanaofika hapa nyakati za usiku hususani wanaotokea mikoa ya mbali ikiwamo Arusha. Tunaomba serikali itazame suala hili kwa kuhakikisha ujenzi unakamilika haraka na kurudisha hadhi ya mkoa," alisema.

Philbert Gozbert, Mkuu wa Idara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji Manispaa ya Bukoba, hivi karibuni wakati akisoma taarifa ya mradi wa ujenzi wa stendi hiyo, alisema katika mwaka wa fedha 2022/23 halmashauri inatarajia kutekeleza mradi wenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 900 kwa muda wa siku 150.

"Shughuli zitakazofanyika katika ujenzi wa mradi huu ni pamoja na ujenzi wa eneo la maegesho ya mabasi 26 kwa wakati mmoja, ujenzi wa mabanda tisa ya kusubiria abiria, uwekaji wa taa tano za nishati ya jua na ujenzi wa mitaro," alisema.

Ujenzi wa stendi hiyo ulianza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2012/13 katika eneo la Kyakailabwa, ulifanyiwa usanifu na kuandaa mchoro kwa makisio ya gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 18.8, chini ya mradi wa uendelezaji wa miji lakini manispaa haikupata fedha za utekelezaji wa mradi huo.

# Uchakavu wa miundombinu chanzo mgawo maji

**Na Alex Sayi,** MASWA

ZAIDI ya wakazi 24,000 wa Mji wa Malampaka Wilayani Maswa Mkoani Simiyu, wanakabiliwa na mgawo wa maji kutokana na uchakavu wa miondombinu inayosambaza huduma hiyo.

Wakazi wa maeneo hayo yenye ongezeko la watu kila uchao kutokana na ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), wanalazimika kununua dumu moja la maji kwa Sh. 500 huku upatikanaji wake ukielezwa kuwa asilimia 45 pekee.

Elizabeth Clement, mkazi wa Malampaka, alisema upatikanaji wa maji katika eneo hilo umekuwa wa taabu hususani kwa wanawake wanaolazimika kuamka saa 9:00 usiku kufuata maji mtoni umbali wa zaidi ya kilomita mbili.

Mariam John, mkazi wa Malampaka, alisema kumekuwa na mgawo wa maji wa hadi siku tatu kwa kila kitongoji, hivyo kuwalazimu wakati mwingine kununua maji au kufuata maji ya mtoni ambayo yanaelezwa kutokuwa safi na salama.

Diwani wa Kata hiyo, Renatus Mashara, alisema hali ya upatikanaji wa maji katika kata yake ni wa shida kutokana na uwepo wa Mgao unaoendelea kwa muda sasa.

"Wananchi wanalazimika kununua maji kwa Sh. 500 lakini tunaishukuru serikali kwa kutuletea mradi mpya utakaosaidia upatikanaji wa maji kwa asilimia 75 kama utasimamiwa vizuri," alisema.


Kuhusu hali ya upatikanaji wa maji katika eneo hilo, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Maswa (MAUWASA), Mhandisi Rafael Mwita, alisema kwa sasa wanaendelea na ujenzi wa mradi wa maji wa dharura ili kuendana na kasi ya ukuaji wa mji.

"Tumefunga mkataba na mkandarasi Savanna Esap Co. Ltd wenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 68.1 ili kuchimba kisima kirefu kimoja. Vilevile tumefunga mkataba na mkandarasi Datti Construction Ltd wenye thamani ya zaidi ya Sh. milion 281.8 kwa ajili ya ujenzi wa tangi la kuhifadhi maji lita 100,000 na ujenzi wa mfumo wa kusambazia maji Malampaka wa kilometa 3," alisema Mhandisi Mwita.



Ukurasa 12

UWT yaamua ‘kununua kesi’ kutoka siasa, hadi jukumu ziada vita ushoga



Ukurasa 13

**Kinachojiri mikutano hadhara ya ACT, zao la ruksa ya Rais Samia**

siasa

JUMATANO APRILI 5, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU



Ukurasa 14

**Uamuzi kihistoria, Rais Paul Kagame kutunza wakimbizi watokao Uingereza**

# Ushindi wa Samia kupitia ugeni wa Kamala, waendeleza historia

• Mwendelezo wa; Nyerere & John F. Kennedy



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwa na mgeni wake Makamu wa Rais wa Marekani, Kamala Harris. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Peter Orwa**

IKO katika hesabu ya wiki sasa tangu ugeni wa Makamu wa Rais wa Marekani nchini, Kamala Harris kwa ziara ya nchi kadhaa Afrika akitokea Ghana, akatua nchini na kutumia siku tatu au wastani wa saa 36, kabla ya kuelekea kwa majirani, Zambia.

Hapana shaka ni ugeni ambao umekweza hadhi ya Tanzaniai katika mambo mengi, hali kadhalika kiongozi wake mkuu Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Marekani ni taifa kigogo duniani na nikirejea michango ya wabunge mbalimbali jana katika Azimio Maalum la kumpongeza Rais Dk. Samia, hawakuficha hilo, wakifafanua ziara ya kiongozi wa hadhi hiyo, inafuatiliwa na dunia nzima.

Tanzania iliteka ramani ya dunia na kwa nafasi ya pekee na rais wake Dk. Samia. Hata inapogeuzwa katika sura ya pili ya shilingi, mkuu wa taifa hilo la Marekani akiwa na ajenda yake ya uchumi na ushirikiano, vivyo kwa Rais Dk. Samia, kukashudiwa mafanikio ndani ya wigo uleule ambao Rais Dk. Samia amekuwa akishughulikia ndani ya nyendo zake za siasa uchumi.

Rais Dk. Samia wakati wote katika siasa za nchini na kimataifa, amekuwa yu mahiri hasa katika wigo wake hususan katika taaluma yake ngazi ya uzamili, mahsusi eneo akihimiza tafsiri ya diplomasia uchumi, hapo akielekeza masoko, uzalishaji na uwekezaji wa kiuchumi nchini.

Hata akifuatiliwa sehemu kubwa ya maamuzi yake ya kiutawala nchini, anajikita kuwezesha maeneo hayo na upatikanaji wa haki katika jamii, ambazo maeneo hayo na uchumi, ni chanda na pete. “Penye utulivu ndiko penye masoko, uwekezaji na uchumi bora.”

Mara zote Dk. Samia anajidhihirisha kwa safari kimataifa katika nchi kama za Afrika Mashariki na Kaskazini, pia akifungua uchumi wa Mashariki na Magharibi mwa dunia, nchi kama China na Ubelgiji.

Ikiwa macho na masikio kuianzia ndani na nje ya mipaka ikiangaza jijini Dar es Salaam, makuu yaliyofikiwa kati ya Dk. Samia na Kamala, daima hazikupashana na msimamo, pia nyendo za rais wa nchini katika miaka miwili aliyo nayo, akishika usukuani kitaifa.

Wawili hao wakitangaza rasmi waliyoamua Ikulu, kwanza ni ujio wa uwekezaji mkubwa wa mamilioni ya dola za Kimarekani nchini, kwa thamani ya shilingi trilioni kadhaa.

Lakini, ikaenda mbali Makamu wa Rais Kamala, akimhakikishia Dk. Samia kwa niaba ya Watanzania, kwamba ni mradi unaofungua ajira na kuhakikishiwa soko la nchini Marekani.

Majumuisho yake yanaangukia katika mustakabali ‘mgeni njoo mwenyeji apone’ vilevile ‘mazungumzo yamelipa’ kwani hitaji analopigania Dk. Samia; masoko, uwekezaji ndani yake kukiwapo faida ya ajira.

**HADHI YA NCHI**

Tanzania ni mwachama katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), vilevile Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Katika mjumuiko huo kuna ushirikiano na ndani yake kuna kuhitaji nafasi ya kumiliki nyendo za uchumi, katikia sura zote kuanzia uwezo katika uwekezaji na kumikliki masoko ya jumuiya.

Hapo katika jicho la pekee, ugeni wa Makamu wa Rais Kamala unabeba tafsiri pana kwa Watanzania, kupitia kofia ya mkuu wao, Rais Dk. Samia, ikianzia na suala la kukubalikia kwa ugeni huo ambao ni kigogo wa funia, katika orodha ya nchi chache duniani.

Vilevile inafungua tafsiri ny-

**INAENDELEA UK.12**

# UWT yaamua 'kununua kesi' kutoka siasa, hadi jukumu ziada vita ushoga

Na Sabato Kasika

HADI sasa kuna mijadala imeshika kasi kuanzia kwenye vyombo vya habari, mitandao ya kijamii na hata kada mbalimbali, ni vita dhidi ya ushoga anaotajwa ni kinyume na maadili.

Ni juzi tu, kumetangazwa kuwapo misukosuko, ya asasi kadhaa za kiraia katika mtihani wa kiserikali katika kashfa hiyo.

Sakata la ushoga limewaibua pia Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), ambao hivi karibuni wametoa kauli kali kutaka watendao hayo, wachukuliwe hatua kali.

Ni kauli katika sherehe zinazoandaliwa na umoja huo za kumpongeza Rais kwa kutimiza miaka miwili madarakani, zilizofanyika jijini Dar es Salaam, wanapotoa ombi hilo, lengo ni kuwalinda Watanzania na maadili yake ili kuwa na kizazi bora cha baadaye.

Mwenyekiti wa UWT Taifa, Mary Chatanda anaiambia Nipashe, umoja huo unasikitishwa na kushamiri ushoga na kwamba wanavikemea kwa nguvu zote.

"Katika sherehe hizo tuliomba kwa Rais kutungwa sheria kali watu wa aina hiyo na tunatamani serikali ifanye marekebisho ya sheria na kuleta nyingine kali ambayo itasaidia kukomesha matendo ya mapenzi ya jinsia moja, kwani yanazidi kushika kasi katika jamii" anasema Mary.

Hapo anafafanua, ni hali inayoweza kuwabana wote watakaobainika kujihusisha na vitendo vya kuingiliana wanaume, tena kinyume na maumbile ili kukomesha uhalisia wake.

"Nirudie tena kwamba kama serikali itaona vyema, basi iwe na sheria ya kuwahasi wote watakaobainika kufanya vitendo hivyo, ili kuokoa kizazi hiki dhidi ya laana ya Mungu, kwani hakuna kitabu chochote kitakatifu kinachoruhusu uchafu huo," anasema.

Anafafanua kwamba, si vyema kwa watu wachache kuendelea kuharibu taifa, badala yake kuwapo utaratibu wa kuwakabili kibaolojia, ili kutoa fundisho kwao na wengine wenye lengo kama hilo.



Mwenyekiti wa UWT Taifa, Mary Chatanda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

Pia, anaeleza kwamba, UWT ipo kwenye hatua za mwisho kuwasilisha ripoti ya uchunguzi wa ukatili wa kijinsia kwa watoto uliofanyika katika vituo mbalimbali vya polisi, ili hatua kali zichukuliwe kwa wahusika.

"Mipango yetu endelevu ni kukemea mapenzi ya jinsia moja (ushoga), huku tukishauri kutungwa kwa sheria kali ambazo zitawaadhibu wahusika ili wakome," anasema.

### WOTE TUPIGANE

Mwenyekiti Mary, anasema mapambano na ushoga, ni jukumu la wote, wakiwamo wanasiasa wanaowataja wana ushawishi kwa umma na kwamba wanaweza kuutumia huo ushawishi, kuukemea.

"Hapa kinachotakiwa ni nia njema tu au utashi wa kisiasa (political will), kwani ni wazi wanasiasa tuna ushawishi kwa umma, tukiutumia kuelimisha kuhusu madhara ya ushoga, tutanusuru taifa lisije kuangamizwa," anasema.

Mary anafafanua, kwa sasa mikutano ya vyama vya siasa imeruhusiwa, ambapo anashauri mojawapo ya ajenda katika mikutano hiyo iwe ni kukemea vitendo vya ushoga badala ya 'kushambulia' na kukosoa serikali tu.

"Kila mmoja wakiwamo viongozi wa dini na jamii kwa ujumla, tukishirikiana na serikali kukemea na kutoa elimu kuhusu madhara ya vitendo hivyo, ni wazi tunaweza kuiponya nchi yetu," anasema.

Mwanasiasa huyo anaorodhesha mengi yanayowaunganisha kama taifa bila ya kujali tofauti za kisiasa katika kukemea mabaya, ikiwamo suala la ushoga na kwamba ni muhimu kushirikiana kulikemea.

Anataja kwenye baadhi ya familia, kumekithiri vitendo vya ubakaji na ulawiti wa watoto, sasa anaiomba jamii kutofumbia macho ukatili huo, kwani ndiko wanakotokea baadhi ya watu wanaojihusisha na ushoga.

Mary anasema, kuna wengi wanaojikuta wanazoea kufanyiwa ukatili huo, baadaye wanakuwa mashoga waliokubuhu, na kwamba ili kuwanusuru, njia pekee ni Watanzania wote kupaza sauti ya kukomesha na ni wajibu wa kila mzazi na mlezi kuzingatia malezi bora, yanayonusuru mtoto.

### JUKUMU LA UWT

Akizungumzia majukumu ya umoja huo, anasema UWT ni chombo kinachounganisha wanawake wa Tanzania, ili fikra za kimapinduzi juu ya ukombozi wao ziweze kuwafikia na kueleweka kokote waliko.

"Vilevile ni chombo cha kujenga na kudumisha amani, kutambua kwamba wakati wowote panapokosekana amani, jamii nzima hasa wanawake na watoto ndio wanaoathirika zaidi," anasema.

Mwenyekiti huyo anataja jukumu lingine la kulinda, kukuza na kuendeleza heshima iliyojengwa kwenye msingi wa usawa kwa taifa zima, kuanzia kwa watoto ambao ni taifa la kesho.

Anasema UWT, chombo cha kuongoza wanawake na kuwashirikisha katika shughuli za kijamii, maendeleo, ulinzi, utamaduni na kujitegemea, pia ni chombo cha kujenga, kukuza na kudumisha fikra za kimapinduzi kwa wanawake wote na kupitia kwao, kwa watoto wote.

"UWT ni chombo cha ukombozi wa wanawake wa Tanzania dhidi ya unyanyasaji, unyonyaji, ukandamizaji, uonevu na mila zote zinazorudisha nyuma maendeleo ya wanawake," anasema.

Anaongeza kuwa ni chombo cha kujenga ushirikiano kati yake na vyombo vingine vyote vinavyoshughulikia maendeleo na ukombozi wa wanawake na unawajengea uwezo wanawake kisiasa, kijamii na kiuchumi.

"Umoja wetu pia ni chombo cha kujenga msingi wa ushirikiano kati ya umoja wa wanawake na jumuiya zote za wananchi na zile zinazojishughulisha na maendeleo ya wanawake na wananchi kwa ujumla," anasema.

Mwenyekiti huyo anataja jukumu lingine la UWT, kuwa ni kushirikiana na wanawake wa Afrika na dunia nzima katika mapambano ya ukombozi wa wanawake na kupinga ubeberu wa aina zote za unyonyaji.

"Kwa niaba ya wanawake wote wanaoitakia nchi yetu mema, tutaendelea kumuunga mkono Rais Samia, katika ujenzi wa taifa na kuleta ustawi wa jamii kwa kupiga vita vitendo vyote vinavyokwenda kinyume na maadili," anasema.

# Ushindi wa Samia kupitia ugeni wa Kamala, waendeleza historia

INATOKA UK.11

ingine ya nchi kukubalika kwamba ni eneo rafiki na uongozi wake wa Rais Dk. Samia, unajimudu kufanikisha yanayodhamiriwa kiuchumi.

Hilo lina marejeo ya jana bungeni, kwenye hoja maalum kumpongeza Rais Dk. Samia, kukawasilishwa na upande wa serikali taarifa ya kuwapo miradi mingi ya uwekezaji kutoka nje iliyo njiani kufanyika nchini.

Vilevile ndani ya mustakabali huo wa kukubalika, ambayo imo hata katika nadharia ya kisiasa, tayari Rais Dk. Samia anajidhirisha kutoka na tuzo kadhaa, hata pongezi zinazofikia utendaji wake.

### ANAENDELEZA ALIYOYAKUTA

Dk. Samia, Rais wa Awamu ya Sita, akianza safari ya uongozi na utendaji, yuko chini ya kivuli cha chama CCM, ambayo falsafa yao ni kupokeza kijiti, kuendeleza msimamo wao.

Hata hivyo, katika hali ya kibinadamu kunakuwapo tofauti katika baadhi ya mambo kati ya nafsi moja na nyingine, ingawa msimamo na itikadi kuu inabaki katika njia ileile.

Hapo ndipo inaporejewa historia ya nchini na Marekani inaenda sambamba na historia ya nchi. Wakati zama za harakati za uhuru, mnamo Julai 1961, Waziri Mkuu (Chief Minister ) wa Tanganyika, Julius Nyerere alikwenda nchini Marekani katika ziara ya kikazi akiambatana na viongozi kadhaa,

Huko alipata nafasi ya kulihutubia Baraza la Wadhamini la Umoja wa Mataifa na akiwa huko akakutana na Rais John F. Kennedy, ambako akaahidiwa fedha za kutekeleza mpango wake wa maendeleo wa miaka mitatu wa Tanganyika huru, kati ya mwaka 1961 baada ya uhuru na 1964.

Ni kipindi hichi kiongozi huyo wa Marekani alikuwa na na msimamo tofauti na viongozi wenzake, akiunga mkono uhuru wa Afrika.

Mnamo Julai mwaka 1963, Rais John F. Kennedy akamualika Nyerere, wakati huo nchi yake sasa ikiwa Tanzania, ambako Rais Nyerere aliwasili hapo kiwa heshima maalum, akishuka kwa helikopta katika viwanja vya Ikulu ya White House. Katika siku kadhaa zilizofuata alikuwa mgeni rasmi katika dhifa za kitaifa na hafla nyingine mbalimbali.

Ni aina hiyo ya mwendelezo, mwaka 2008, Tanzania ikiwa katika uongozi wa awamu ya tano, chini ya Rais Jakaya Kikwete, Rais wa Marekani George W. Bush naye akatua nchini, jijini Dar es Salaam, akizuru katika Hospitali ya Amana na barabara ya mtaa huko Manzese.

Ikumbukwe, akawa na mchango katika Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), ambako Amana ni mwenyeji na serikali ikaungwa mkono na Marekani, ikizingatiwa ilianza kutekelezwa mwaka huo, baada ya kupitishwa mwaka mmoja kabla, 2007.

Ni hadi leo urafiki huo wa kihistoria kati ya marais John F. Kennedy na Mwalimu Nyerere, huendelea kuadhimishwa katika namna tofauti, ikiwamo kati ya Ubalozi wa Marekani na Watanzania, kupitia Idara ya Makumbusho ya Taifa.

# Kinachojiri mikutano hadhara ya ACT, zao la ruksa ya Rais Samia

**Na Julieth Mkireri, aliyekuwa ziarani**

NI baada ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kufikia maridhiano na vyama vya siasa nchini, kilichoko sasa ni 'ruksa mikutano ya hadhara.' Hapo ndipo ACT Wazalendo inatumia fursa kukutana na wananchi.

Chama hicho kinaongozwa na Zitto Kabwe, ambaye ana mzizi kutoka Chadema, huku Mwenyekiti ni Juma Haji Duni maarufu 'Mjelajela' naye mwenye mzizi wa chama cha CUF, mwezi uliopita walianza mikutano kwenye mikoa mbalimbali nchini kuelezea ahadi zao kichama.

**MKOANI TANGA**

Wakiwa jijini Tanga katika uwanja wa Tangamano, kiongozi Zitto Kabwe, anasema baada ya maridhiano, wameamua kukutana kuelezea ahadi zao kwa wananchi.

Chama hicho kinasema kuna uwakilishi mdogo bungeni na wameamua kushughulika kero za umma, kwa kuunda baraza kivuli la mawaziri, watakaosemea wananchi kero zao serikalini.

"ACT Wazalendo inawaomba wakazi wa Tanga kuungana kufanikisha katika hili na mkoa wa Tanga na Pwani, ni waathirika wa matendo ya utekaji, mauaji na watu kubambikiziwa kesi," anatamka, akisisitiza ni mambo chama chao lazima kiyazungumze.

Kuhusu usambazaji mbolea, Zitto anaiasa serikali: "Unaweza kutoa mchango mkubwa kwenye kushusha uzalishaji nchini, hususani kwa mazao ya chakula au kushusha mfumo wa bei baada ya mavuno".

Anasema kwa misimu ya miaka miwili mfululizo, upatikanaji mbolea na pembejeo zingine za kilimo kwenye misimu miwili ya sasa, unakabiliwa shida ya kupanda bei, hata kuishia kwenye bei kubwa za vyakula.

"Serikali ilichukua pendekezo letu na hii kwetu ilikuwa hatua muhimu na ilibeba matumaini makubwa kwa wakulima kwa matarajio ya kupunguziwa gharama zilizokuwa zinaendelea kupanda na kuhakikishiwa urahisi wa upatikanaji mbolea.

"Wakala wengi walikuwa wanapatikana maeneo ya mijini, wakati wakulima wapo vijijini, wakulima walilazimika kutumia gharama zaidi kupata mbolea, pia kulikuwapo tatizo la uchache wa wakala na wengine wasio waaminifu kusambaza mbolea bandia," anasema.

**JUMA DUNI HAJI**

Mwenyekiti wa Chama hicho, Juma Duni Haji, anaeleza mchakato wa upatikanaji Katiba Mpya, akiitaka serikali kuhakikisha unakamilika, kabla ya kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, ili kuendana na matakwa ya umma.

Anasema mpaka sasa serikali haijaweka hadharani siku mchakato wa sheria ya mabadiliko ya katiba utakaowasilishwa bungeni kwa ajili ya kutoa fursa ya sheria hizo kutumika katika upatikanaji wa katiba mpya.

"Baada ya Rais kujibu hoja za wapinzani kuhusiana na mabadiliko ya siasa za kidemokrasia, hoja kuu iliyojitokeza ni mabadiliko ya katiba na vyama vya upinzani walielezea hili, kwa kutaka sheria ya uchaguzi sheria ya vyama vya siasa, sheria ya polisi iliyokuwa ikitusumbua sana wakati wa mikutano, sheria ya uchaguzi na sheria ya kura za maoni," anasema.

Juma Duni anaongeza katika maoni ya chama hicho katika kikosi kazi cha Rais, kinachoendelea kupelea maoni sasa, wameeleza njia na hatua nzuri za kufikia mabadiliko hayo, kwa serikali inatakiwa kutumia mawazo hayo kwa ajili ya kuipata Tanzania iliyo bora.

"Tunataka utaratibu wa namna ya sheria hizo zitakavyobadilika ili ziwahi na kutumika katika uchaguzi wa 2024 na 2025, tunataka kuona sheria hizi zinabadilishwa kwa kuanzia kupata baraka zake katika Baraza la Mawaziri, sisi tumesema kule Zanzibar, Dar es Salaam, Tanga na mikoa mingine tuliyopita muda rasmi wa kufikia mabadiliko" anasema.

Hata hivyo, Rais Dk. Samia mbali na kuwa na tume inayokusanya maoni kuhusu sheria na vyombo vyake nchini, ameahidi kufanyia kazi maoni kuhusu katiba ya nchi

**MAKAMU MWENYEKITI**

Makamu Mwenyekiti wa ACT- Wazalendo (Bara), Dorothy Semu, anashauri suala la kupanda bei za vyakula, lipewe kipaumbele, hata linasababisha baadhi ya familia kuishia kula mlo mmoja kwa siku.

Dorothy Semu anasema, bado Serikali haijaleta ufumbuzi kuhusiana na suala hilo, hali inayowaumiza zaidi wananchi wenye vipato vidogo.

"Serikali ilisema imeagiza chakula nje isimamie kiingie sokoni kunusuru wananchi na kupanda kwa bei, pia tunaitaka serikali iachie chakula kilichopo kwenye ghala kutokana na hali ya wananchi kuwa ngumu na kuendelea kusumbuliwa na baa la njaa" anashauri.

Makamu Mwenyekiti huyo, anaongeza kuwa wakulima wa ndani wanatakiwa kuwezeshwa kufanya kilimo cha kisasa na kupata pembejeo kwa gharama nafuu, ili wazalishe kwa wingi na kupunguza gharama za uzalishaji, utakaowafanya kuuzia wananchi kwa bei rafiki.

"Serikali inatakiwa pia kuwezesha wakulima kutoka kilimo cha msimu na badala yake watumie njia ya kilimo cha umwagiliaji na kulima kwa mwaka mzima na ijenge uwezo wa kuhifadhi chakula cha kutosha kupitia mradi wa Taifa ( Mamlaka ya Uhifadhi wa Chakula NFRA)" anasema.

**KATIBU WA CHAMA**

Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu, akiwa mkutanoni Tunduru mkoani Ruvuma, anasema serikali inatakiwa kufanya maridhiano kwenye migogoro ya wakulima na wafugaji kama inavyofanya katika sekta nyingine.

Aidha anasema, serikali inatakiwa kutumia majukwaa rasmi kama Kamati za Ushauri za Wilaya na Mikoa (RCC na DCC) kujadili masuala hayo kwa upana na kuhusisha wawakilishi wa wakulima na wafugaji, ili kujenga maelewano miongoni mwao.

"Wakati Rais anaongoza maridhiano kwenye siasa yanapaswa kushuka pia kwenye kila sekta, matumizi ya mabavu katika kunusuru migogoro ya wakulima na wafugaji, ni jambo la kikoloni wanapaswa kufanya kama ilivyokuwa kwenye siasa," .

"Athari za migogoro hiyo imesababisha kuwa na mapigano baina ya wakulima na wafugaji, mapigano yanayohatarisha amani na usalama nchini,tatizo hili limekuwa kubwa zaidi katika Wilaya za Tunduru, Ruangwa, Nachingwea, Liwale, Lindi Vijijini na Kilwa"anaeleza.

Katibu Mkuu huyo, anasema hisia walizonazo wananchi wenyeji (wakulima) kwenye maeneo hayo dhidi ya wafugaji na viongozi wa Serikali ni dhairi kuna chuki baina ya makundi hayo na kwamba kwa hali hiyo chama hicho kinatoa maoni ya kushughulikiwa mapema migogoro hiyo.

"Tunafahamu kuwa wakulima na wafugaji ni makundi ya uzalishaji yanayotegemeana na kila mmoja anamuhitaji mwenzie lakini, uamuzi wa Serikali kuwaruhusu wafugaji kwenye ardhi ya Kilimo bila kuwashirikisha wanavijiji wenyewe ni kupandikiza mapigano isiyo ya lazima" anasema.

Shaibu anaisisitiza serikali kuwawekea wafugaji mazingira mazuri ya kufugia kwa kujenga malambo ya kunyweshea mifugo na kuwatengea maeneo ya malisho, utaratibu wa sasa unasababisha vurugu kwani wapo wafugaji wanalisha mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima na pia wananyweshа mifugo kwenye vyanzo vya maji ambavyo vinahudumia.

Chama hicho kimefanya mikutano katika mikoa ya Dar es Salam, Tanga, Pwani, Lindi, Mtwara,Ruvuma, Tabora na Kigoma ambapo walitumia nafasi hiyo kutambulisha Mawaziri Kivuli wa chama hicho.



Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe (kulia) katika nyendo za kisiasa,. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**




Juma Duni Haji, Mwenyekiti wa ACT Wazalendo.

# Uamuzi kihistoria, Rais Paul Kagame kutunza wakimbizi watokao Uingereza

**Na Ani Jozeni**

NI mara nyingi katika umaarufu wake katika ujasiri wa siasa, ni ngumu sana kutofautisha taifa la Rwanda na Rais wake Paul na hasa alivyo maarufu na historia yake, katika nyendo na umaarufu wake kisiasa.

Hivi karibuni, vyombo vya habari Ulaya na Afrika vilifuatilia ziara ya Waziri wa Mambo ya Ndani wa Uingereza, Suella Braverman nchini Rwanda, kufanikisha mipango ya kuhamisha wakimbizi au wahamiaji wasiotakiwa nchini Uingereza.

Serikali ya Rwanda katika kujiamini zaidi, ikalipokea hilo wahamiaji hao kutafutiwa makazi. Ni wakati Rwanda ilipojiunga na Jumuia ya Madola, ikiwa haiko tayari kuendelea na sura yake ya jadi ya 'kuwa mwanachama wa nchi wakoloni wa Ufaransa au Francophonie'.

Taifa hilo ni nchi yenye mwelekeo wa lugha ya mfungamano ya utamaduni na Ufaransa na mtawala wake katika ukoloni, kwani Ufaransa na Ubelgiji zina utamaduni sawia.

Utayari wa Rwanda kupokea wakimbizi hao una thamani katika maeneo mawili;kwanza kuwawezesha kuanza maisha mapya kwa walioona wamekwama

kwa sababu ndoto zao ni kujiunga na jamii za Ulaya, iwe Italia, Ugiriki, Uingereza, Ufaransa au Ubelgiji. Upinzani mkali ukatolewa kwao, hivyo mpango huo kwenda Rwanda ukaja 'watake wasitake' au warudishwe makwao.

Vikundi vya haki vya binadamu vimejitahidi kuweka pingamizi mahakamani nchini Uingereza vikakwama, sheria ikisema hilo lipo katika madaraka ya serikali, au katika uwezo wa nchi mbili kuliamua.

Eneo jingine, ni hitaji la nchi ndogo kuwa msaada kwa mataifa makubwa, yaani ushirikiano wa pande mbili zinazohitajiana, siyo tu wadau wa maendeleo au watoa misaada, kila wakati wakitokea Ulaya kuisaidia Afrika.

Rwanda imeamua kuonyesha mfano wa kuisaidia Uingereza katika mazingira, ambayo isingeweza kusaidiwa na nchi ya Ulaya. Upinzani wa kuwapo wakimbizi, wanabadili sura ya nchi na hali yake ya jadi. Ni suala gumu kisiasa kwa Ulaya na hata Marekani.

Wapinzani wa mpango huo ni wale ambao ukiwaambia Uingereza ni nchi ya Wazungu wanakuona mbaguzi, wakati kila nchi inajivunia utaifa, pale inapokaribisha wageni.

Jitihada za kuhamia kwingine zimepamba moto katika nchi nyingi ambazo hazina uwezo wa kihisia, kiimani, kinadharia au kisiasa wa kubadili mifumo yao ya jamii kuwezesha mabadiliko ya haraka na kuishi kama Ulaya.



Rais Paul Kagame. **PICHA: MTANDAO.**

Watawala na wasomi Afrika hawahangaishwi na sera gani zitawezesha hali kama hiyo kuwepo Afrika. Wanajitahidi kulinda Afrika ibaki na mali zake 'zisiporwe' na watu wa nje, halafu kila mmoja anajitahidi awatangulie, na hata awazodoe, ndugu zake kwa mali.

Licha ya matumizi ya kawaida ni vigumu kusema kuna kitu kama asasi za kiraia barani Afrika, ambako jamii inaona kero kwa wizi wa mali ya umma, uonevu na kujinufaisha, kunakozuia uwezo wa kufikiria mifumo au sera bora zaidi.

Waafrika na Waarabu wamefungwa katika dhamira zao kuhusu watakacho katika maisha ya jamii, hivyo maendeleo yanapatikana kwa kujikongoja, na balaa kubwa za kutoaminiana.

Ni katika mazingira hayo ambako baadhi ya vijana na hata wenye umri wa kati, mara kadhaa wanafanya kila wawezalo, hata kuuza amana ndogo walizo nazo katiambaadjio ya nchi, kupata fedha kuingia katika safari hatarishi za kuvuka Jangwa la Sahara na Bahari ya Mediterannean hadi fukwe za nchi za Ulaya.

Wakifika huko yapo makundi ya watetezi kwanza kuwaokoa baharini, kuwatafutia hifadhi halafu na msaada wa kisheria kujieleza ili wabakizwe Ulaya.

Taarifa za televisheni za Marekani zinasema takriban asilimia 90 ya waomba hifadhi nchini humo wanakataliwa. Hivyo wanaishia jela, wapewe fedha kidogo ya kujikimu, wapandishwe kwenye ndege kurudishwa makwao, au nchi waliyotumia kuingia.

Hoja ya msingi ya wapinzani wa mkakati wa Rwanda na Uingereza ni kuwa Uingereza inaikana hali ya ukimbizi au kuomba hifadhi, wakati kinachotokea hapa ni kuikimbia mifumo mibovu ilyojaa umaskini na mikwamo ya kisiasa inayoleta mafarakano au vita isiyoisha.

Wengi kati yao wamekuwa wakipinga 'kupendelewa' kwa wakimbizi kutoka Ukraine kuwa wanatofautishwa na wale wa Syria au Afghanistan.

Halafu nchi kama Marekani 'zikijiongeza' kuingia humo kurekebisha hali, dunia nzima haiko tayari kwa uvamizi kama huo. uliberali wa kimataifa unataka nchi ziamue jinsi zinavyojiendesha.

Labda ni kudhani kuwa nchi hizi ni mbumbumbu kwani demokrasia inawazuia kulinda ustahimilivu na utengamano wa aina ya jamii waliyo nayo, au labda umbumbumbu ni kudhania kuwa tukiharibu Afrika tutaenda Ulaya. Suala la msingi ni kama itafika siku Afrika ibadilike.

Kwa maana hiyo Rwanda kutoa mwanya wa mahali pa kuhamishia wakimbizi ni msaada muhimu kwa serikali ya Uingereza, kwani inajua Waingereza wakiendelea kujaziwa wakimbizi watachagua serikali za kifashisti kuwaondoa, na utengamano kijamii uwe mashakani.

Wapo wengi wasiopenda mifumo ya kibepari na utawala wa kidemokrasia Ulaya, wenye mipango ya mabadiliko makubwa kijamii na kudhania kuwa demokrasia itadumu hata baada ya hapo, na wengi tu hawajali hatari zinazotokana na kupokea mawimbi ya wakimbizi.

Rwanda inajua hawatafurika kwao, na watakaokuja watainigiza fedha za mfukoni kwao na za Uingereza kuwezesha uhamiaji huo. Ni ku-beti kimkakati wakiona kuna faida ya wazi.



HABARI DODOMA

## Watakiwa kujijengea tabia ya kufanya usafi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

TABIA ya kupenda kufanya usafi wa mazingira mara kwa mara kwenye maeneo ya makazi itasaidia kuepukana na magonjwa ya mlipuko badala ya kusubiri kutozwa faini na kushurutishwa na viongozi wa serikali, imeelezwa.

Msimamizi wa Usafi Jiji la Dodoma, John Lugendo, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na wananchi wa kata ya Chamwino jijini hapa baada ya kumalizika kwa usafi wa mazingiri unaofanyika kila mwisho wa mwezi.

Lugendo alisema Watanzania wanatakiwa kujijengea tabia ya kupenda kufanya usafi wa mazingira bila kusubiri kushurutishwa na viongozi au kutozwa faini. Alisema Dodoma ni makao makuu ya nchi, hivyo inapaswa muda wote kuwa na hali ya usafi badala ya kusubiri suala hilo lifanywe na serikali.

"Naomba kuwasisitizia kuwa ninyi wakazi wa Chamwino kuwa kila mwishoni mwa mwezi kiratiba kwa nchi nzima ni siku ya kufanya usafi, hivyo tusisubiri mpaka mwisho wa mwezi bali tuwe na tabia ya kufanya usafi huo.

"Na usafi uwe wa kuanzia mtu mmoja mmoja kwa maana ya kujenga misingi ya utunzaji wa mazingira na usafi wa mazingira kwa njia yoyote na kutambua kuwa usafi ni sehemu ya mazingira ya afya na usafi unavutia zaidi wawekezaji," alisema.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Chamwino, Lucas Venance, alisema moja ya kero ambazo zimekuwa zikikwamisha usafi wa mazingira ni uwapo wa wadudu wakali kama vile nyoka.

Alisema maeneo hayo ya kufanya usafi ikiwamo kwenye vichaka yamekuwa hatari kwa wananchi kutokana na kukutana na wadudu hao hatari.

Kutokana na kero hizo, aliiomba Halmashauri ya Jiji kusaidia vifaa vya kujikinga na wadudu hao kama vile mabuti na dawa ili kufanya kazi ya usafi kwa kujiamini na ufanisi zaidi.

Alisema maeneo mengi yakiwamo makaburini na kwenye vichaka kunakofanyika usafi wa mazingira mara nyingi wananchi wamekuwa wakifanya kwa hofu ya kuumwa na wadudu hao.

"Wananchi wangu wamekuwa wakilalamika wanapofanya usafi wa mazingira kama maeneo ya makaburini wamekuwa wakikutana na nyoka hali ambayo imekuwa ikiwatia hofu ya kuumwa.

"Naiomba ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji kuliangalia hili kwa jicho la pili ili tusikwamishe watu kujitokeza kwa kuhofia maeneo wanayofanyia usafi wanaweza kukutana na wadudu hao hatari.

**Moja ya kero ambazo zimekuwa zikikwamisha usafi wa mazingira ni uwapo wa wadudu wakali kama vile nyoka.**

# Askofu ataja kichocheo kuenea matendo ushoga

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

**Taasisi hiyo iliundwa na makatibu tawala wa mikoa na wakurugenzi wote wa mamlaka za serikali za mitaa Tanzania Bara pamoja na wanachama wengine waliopo nje ya OR-TAMISEMI.**

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Maombi na Maombezi kwa Mataifa Yote (RUTACH) Living Mwambapa, amesema vitendo vya ushoga, ubakaji na ulawiti chanzo chake ni wazazi na walezi kuiga utamaduni wa nchi za Magharabi.

Mwambapa alisema hayo juzi alipokuwa akihubiri kwenye ibada maalumu kwa ajili ya toba ya kuliombea taifa na kanisa hilo.

Alisema kwa sasa matukio ya kikatili kwa watoto, vikiwamo vitendo vya ushoga, ulawiti, ubakaji na mauaji vimekua kwa kasi kutokana na wazazi na walezi kutokuwa na muda wa kukaa na watoto kwa ajili ya kuwapatia malezi ya kiroho.

Askofu huyo alisema wazazi na walezi wengi wamepoteza maadili ya kitanzania na kujikuta wakijitumbukiza kwenye desturi za mataifa ya Magharibi jambo ambalo linasababisha watoto kutokuwa na hofu ya Mungu.

Baadhi ya wazazi na walezi, alisema hawana muda wa kukaa na watoto kwa ajili ya kujua matatizo wanayokutana nayo badala yake wamekuwa wakiwaachia mabinti wa kazi za ndani.

Pia alisema vitendo hivyo vinapotokea kwenye familia, imekuwa vigumu kuwatia hatiani wanaobainika kutokana na wanandugu kuelewana wao kwa wao bila kwenda katika vyombo vya sheria.

"Kwa sasa kumeibuka suala baya sana la vijana wengi kuwa mashoga. Ukifuatilia michezo hiyo inaanzia nyumbani na ukimuuliza anakwambia ni baba mzazi, baba mdogo, kaka, mjomba na ndugu wa karibu.

"Wazazi au walezi nao ukiwauliza juu ya tatizo hilo wanakwambia hawajui limeanza lini na wapi lakini chanzo kikubwa ni wao wenyewe kwa kutokuwa na muda wa kukaa na watoto wao kuwasikiliza na kujua changamoto wanazokumbana nazo,' alisema.

"Muda mwingi utamkuta mtoto anakuwa karibu na dada wa kazi lakini wazazi au walezi muda mwingi wapo kwenye mitandao, wapo katika miangaiko ya kimaisha jambo ambalo linachangia kuwepo kwa matukio hayo ya hovyo" alisema Askofu Mwambapa

Askofu huyo pia alibainisha kuwa watu wengi kwa kutokuwa na hofu ya Mungu, kumechangia kwa kiasi kikubwa kuviona vitendo vya kishoga ni suala la kawaida bila kujua kuwa ni machafuko mbele za Mungu.

"Kwa mtu yeyote anayekubaliana na ushoga anastahili kupata pigo kutoka kwa Mungu na hiyo haijalishi ni kiongozi yeyote wa ngazi ya juu wa nchi yoyote na cheo chake.



Mbunge wa Babati Vijijini, Daniel Sillo akiwashukuru wabunge baada ya kuchaguliwa kuwa mmoja wa wenyeviti watatu wa Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Bajeti halmashauri za Singida yaongezeka

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

BAJETI ya ndani ya halmashauri za mkoa wa Singida imeongezeka kutoka Sh. bilioni 16.898 mwaka 2020/21 hadi Sh. bilioni 22.441 mwaka 2022/223 sawa na ongezeko la asilimia 33.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alisema hayo juzi wakati akitoa taarifa ya mafanikio ya serikali ya awamu ya sita katika kipindi cha miaka miwili tangu Rais Samia Suluhu Hassan aingie madarakani.

Alisema kwa mwaka wa fedha wa 2022/23 serikali kuu imeidhinisha bajeti ya Sh. bilioni 1.053 kwa ajili ya kuwalipa madiwani, watendaji wa kata na vijiji posho kila mwezi.

Serukamba alisema utaratibu wa serikali kuu kuwalipa madiwani na watendaji wa kata na vijiji posho hizo haujawahi kufanyika katika awamu zilizopita jambo ambalo limewapa ari ya kufanya kazi kwa bidii watendaji hao.

Alisema katika kipindi hicho sekta ya elimu imeimarika ambapo mkoa umepokea Sh.bilioni 16.043 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 809 ya shule shikizi, msingi na sekondari.

Kuhusu sekta ya afya, alisema mkoa wa Singida ulipokea Sh. bilioni 6.650 kwa ajili ya kujenga hospitali nne mpya za wilaya katika halmashauri za wilaya ya Ikungi, Mkalama, Singida na Itigi na ukarabati wa hospitali ya wilaya ya Manyoni.

Pia alisema kwa kipindi hicho pia mkoa ulipokea Sh.bilioni 8.900 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya Afya 20 kupitia tozo za miamala ya simu.

Alisema katika sekta ya maji, uzalishaji umeongezeka kutoka wastani wa lita 8,380,650 kwa mwaka 2020/21 hadi kufikia lita 9,805,514 kwa siku kwa mwaka 2022/23.

Serukamba, alisema ongezeko hilo limetokana na kukamilika kwa miradi mipya ya maji yenye thamani ya sh.838,660,368.





# Afya wanafunzi hatarini ukosefu wa vyoo shuleni

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

AFYA za zaidi ya wanafunzi 2,000 na walimu 25 wa Shule ya Sekondari Legico katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, ziko hatarini kutokana na uhaba wa matundu ya vyoo shuleni hapo.

Hayo yalisemwa juzi na Mwenyekiti Mtaa wa Majengo, Evance Mwambebula, wakati wa hafla ya kupokea mifuko 50 ya saruji iliyotolewa na Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Akson, na kukabidhiwa na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa shule hiyo.

Alisema kwa sasa shule hiyo ina matundu 11 tu ya vyoo ambayo yanatumiwa na zaidi ya wanafunzi 2,000 na walimu 25, idadi ambayo alisema haikidhi mahitaji ya watu hao.

**Kwa sasa shule hiyo ina matundu 11 tu ya vyoo ambayo yanatumiwa na zaidi ya wanafunzi 2,000 na walimu 25, idadi ambayo alisema haikidhi mahitaji ya watu hao.**

Mwambebula aliongeza kuwa awali shule hiyo ilikuwa kilabu cha pombe za kienyeji tangu mwaka 1954 na mwaka 2000 wananchi walilazimika kubadili matumizi na kutumia nguvu kazi na kuhamasisha kila kaya kuchangia Sh 2,000 na kujenga vyumba 16 vya madarasa.

Licha ya jitihada hizo za wananchi, Halmashauri ya Jiji la Mbeya imeshindwa kuboresha miundombinu ya vyoo kwenye shule hiyo.


"Mkuu wa Wilaya, shule hii bado ina miundombinu ya vyumba vya madarasa na vyoo vilivyokuwa vikitumika kunywea pombe huku majiko yakiwa ofisi za walimu. Hii ni aibu jiji limeshindwa kutenga fedha kubomoa na kujenga mengine kuunga mkono juhudi za wananchi tuliojenga vyumba 16," alisema Mwambebula.

Mkuu wa Shule hiyo, Bujo Kasambala, alisema ukosefu wa matundu ya vyoo na wigo vinashusha morali ya walimu kufundisha kutokana na mazingira hayo kutokuwa rafiki.

Kasambala aliongeza kuwa mbali na kuwepo kwa vikwazo hivyo walipokea Sh. milioni 40 kutoka Mpango wa Maendeleo na Ustawi wa Mapambano dhidi ya UVIKO -19 ambazo zilitumika kujenga vyumba viwili vya madarasa na ofisi moja ya walimu.

Malisa alisema wamepokea malalamiko hayo na kwamba watayafanyia kazi na kuahidi kuchangia matofali 500 kwa ajili ya ujenzi wa wigo.

Abigael Mwampashi, mkazi wa Mtaa wa Majengo, alisema kitendo cha serikali kutelekeza shule hiyo ni kwenda kinyume cha matakwa ya Rais Samia Suluhu kuwekeza katika sekta ya elimu nchini.




Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa (wa pili kulia), akikabidhi mifuko 50 ya saruji kwa niaba ya Mbunge wa Jimbo la Mbeya mjini ambaye pia ni Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (hayupo pichani), kwa Uongozi wa Shule ya Sekondari Legico, kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa shule, wilayani humo juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Ujenzi kituo forodha wafikia asilimia 88

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

UJENZI wa mradi wa kituo cha pamoja cha forodha cha Kasumulu katika mpaka wa Tanzania na Malawi wilayani Kyela, umefikia asilimia 88 na hadi kukamilika kwake utagharimu Sh. bilioni 26.

Kwa mujibu wa Meneja wa Wakala wa Barabara Tanroad Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Masige Matari, mradi huo umefikia hatua nzuri na kwamba unatekelezwa na mkandarasi wa kampuni ya M/s China Geo Corparation.

Mhandisi Masige alisema awali walitarajia mradi huo kukabidhiwa serikali Machi 23, mwaka huu, lakini kutokana na vikwazo mbalimbali wamelazimika kuongeza muda ili kukamilika kwa viwango vinavyotakiwa.

"Kukamilika kwa mradi huu kutakuwa kichoche ukuaji wa uchumi kwa sababu wafanyabiashara watapata fursa ya kubadilisha na kuuziana bidhaa za aina mbalimbali kwenye ukanda huu wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kupitia mpaka wa Kasulumu ambao unaunganisha nchi za Tanzania na Malawi," alisema.

Masige aliongeza kuwa katika kufungua fursa za kiuchumi mkoani Mbeya, TANROADS inatekeleza miradi mingine ya kimkakati ambayo ni ujenzi wa barabara njia nne yenye urefu wa kilometa 32 utakayogharimu Sh, bilioni 138, ujenzi wa jengo jipya la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimtaifa wa Songwe (SIA) uliogharimu zaidi ya Sh. bilioni 14.

Awali Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema kukamilika kwa miradi ya hiyo ya kimkakati kutafungua fursa za kiuchumi katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na kuwa lango la kiuchumi.

"Uwanja wa Ndege wa Songwe tunatarajia kupokea ndege kubwa ya mizigo yenye uwezo wa kusafirisha tani 54 za mizigo kwenda mataifa mbalimbali. Ni wakati sasa wananchi kutumia fursa hiyo kuzalisha mazao ya kimkakati yaliyo na tija," alisema.

Mmoja wa wafanyabiashara, Ahobokile Boniface, alisema uwapo wa miradi hiyo ya kimkakati utafungua fursa kibiashara na kuboresha uhusiano baina ya Tanzania, Malawi na Zambia kupitia bidhaa mbalimbali zinazozalishwa.

# RC Homera apiga marufuu ununuzi parachichi mbichi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amepiga marufuku kampuni na wafanyabishara wanaoingia kwenye mashamba ya wakulima wa wilaya ya Rungwe kununua maparachichi ambayo hayajakomaa.

Akizungumza wilayani Rungwe jana, Homera alisema kitendo hicho kimekuwa kikisababisha kupoteza sifa ya maparachichi yanayozalishwa mkoani Mbeya na kuagiza hatua zianze kuchukuliwa kwa wafanyabiashara wa aina hiyo.

Pia aliiagiza kamati ya ulinzi na usalama mkoa kuanza kufuatilia na watakaobainika watachukuliwa hatua ikiwepo kufutiwa leseni na mzigo kutaifishwa.

Homera alisema kumekuwapo na tatizo kwa baadhi ya wanunuzi serikali inapopiga marufuku wao wanatafuta njia za panya kuingia na kununua matunda ambayo hajayakomaa katika mashamba ya wakulima.

"Hii ni mara ya mwisho kuzungumzia hili. Nimetoa maelekezo mara kwa mara kupiga marufuku lakini wafanyabiashara wamekua wakaidi sasa kinachofuata ni kusakwa na kuchukuliwa hatua," alisema.

Homera pia aliwaonya wakulima kuacha tabia ya kuuza kwa bei ya hasara maparachichi na badala yake watoe ushirikiano kwa serikali kuwafichua wanunuzi wa kampuni na wafanyabishara wakaidi.

Bosco Alinanuswe, alisema wafanyabiashara wanafanya hivyo kutokana na wakulima kutoheshimu makubalino yao ambayo yanataka wasiuze maparachichi ambayo hayajakomaa.

Aliongeza kuwa tamaa ya pesa za haraka imechangia kwa kiasi kikubwa wafanyabiashara kuuza parachichi ambazo hazijakomaa kwa sababu ya kurubuniwa na wafanyabiashara.

"Ili suala hili likome lazima viongozi wetu watunge sheria ndogo za kuwabana wale wote watakaobanika kununua au kuuza maparachichi ambayo hayajakomaa tena yakiwa shambani. Hali hii inasababisha soko letu kuharibika na kuonekana sisi hatuzalishi maparachichi yenye ubora kwa tamaa za watu wachache,' alisema Alinanuswe.





# UN Women yazindua programu kwa wasichana kupaa kidijitali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Usawa wa Kijinsia na kuwawezesha Wanawake (UN WOMEN) limezindua programu ya kitaifa ya Binti Digitali, inayofadhiliwa na ubalozi wa Ubelgij.

Lengo la programu hiyo ni kuwawezesha watoto wakike kujumuishwa katika masuala ya sayansi, teknolojia na hisabati.

Uzinduzi wa programu hiyo ulifanyika jana visiwani Zanzibar katika kituo cha ubunifu kilichoko Jang'ombe na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Anna Athanas Paul.

Akizungumza baada ya uzinduzi huo, Naibu Waziri huyo alisema lazima mtoto wa kike kufikia katika usawa katika masuala ya kidigitali.

Anna alisema wasichana wako nyuma kupata fursa za masuala ya kibunifu na kidigitali hivyo ni vyema wakajumuishwa katika masuala ya sayansi, teknolojia na hisabati.

"Nilifurahi sana kutambua kwamba "Programu ya Binti Dijitali" inayotekelezwa kupitia mpango wa 'African Girls Can Code Initiative PhaseII' inawalenga wasichana wadogo wenye umri wa kati ya miaka 17 na 25 na hili litabaki kuwa kundi la umri kama tunavyoona hapa leo," alisema.

**Wasichana wachache wanaoandikishwa katika masomo ya sayansi na wanawake wana nafasi ndogo katika taaluma za sayansi na uhandisi.**

Naibu Waziri huyo alipongeza juhudi za mpango huo wa kukuza elimu inayozingatia jinsia ambayo inatambua na kujibu mitindo na mahitaji maalum ya wasichana kujifunza na itasaidia kuvutia wanawake na wasichana wengi zaidi kufuata taaluma katika nyanja hizo.

Alisema wanawake na wasichana wana haki sawa ya kufikia ulimwengu wa kidijitali, teknolojia ambayo inachangia kubadilisha kanuni za kijamii, kukuza sauti za wanawake, kusonga mbele dhidi ya unyanyasaji wa mtandaoni kama sehemu ya unyanyasaji wa kijinsia na kufikia maendeleo ya nchi.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Dk. Mwanahamis Adam, alisema lengo la programu hiyo ni kuwafanya wasichana kuwa na uwezo wa kutumia teknolojia katika maisha yao na kuisaidia nchi yao.

Alisema wizara ya elimu itafuatilia uendeleaji wa programu hiyo ili kuhakikisha maendeleo yanapatikana na kufikia lengo la program hiyo

Mwakilishi wa UN Women Tanzania, Hodan Addou, alisema wasichana wachache wanaoandikishwa katika masomo ya sayansi na wanawake wana nafasi ndogo katika taaluma za sayansi na uhandisi.

Balozi wa Ubelgij nchini, Peter Huyghebaert, alisema wataendelea kushirkiana na Tanzania kuhakikisha usawa wa kijinsia unakuwa na kuimarika.

Mtaalamu wa programu hiyo kutoka UN Women, Lilian Mwandonga, alisema watoto wa kike wengi wanafanya vizuri katika teknolojia lakini kitakwimu wanaonekana wako nyuma ikilinganishwa na watoto wa kiume katika kupata fursa.

Alisema programu hiyo itasaidia kuongeza ushiriki wa watoto wa kike katika teknolojia na wasichana 50 watapatiwa mafunzo hayo ili kutengeneza teknolojia mbalimbali ambazo zinatumika katika uchumi wa kisasa ikiwamo kuwaunganisha wanawake katika masoko.




Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Anna Atanas Paul (wa nne kulia), akizindua programu ya kitaifa ya Binti Kidigitali, mjini Zanzibar jana, iliyoanzishwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Usawa wa Kijinsia na kuwawezesha Wanawake (UN WOMEN), inayofadhiliwa na Ubalozi wa Ubelgiji nchini, ili kuwawezesha watoto wakike katika teknolojia. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Ataka historia za wastaafu ziandikwe

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed (pichani chini), amesema katika kuwaenzi viongozi wa kitaifa, kuna haja ya kuandikwa historia zao ili vizazi vipate kumbukumbu sahihi za viongozi hao.

Alisema hayo jana Kiembesamaki, Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja wakati wa ziara na dua katika kaburi la Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Polisi, Khamis Daruwesh Mdingo na Kanali Mstaafu Seif Bakari Omar.

Kila nchi, alisema ina utaratibu wake wa kuwaenzi viongozi wake kutokana na sababu zake na wao ndio chimbuko la Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 ambayo yalileta uhuru, usawa na maendeleo ya kijamii na kiuchumi ambayo matunda yake yanaonekana hadi sasa.

Alisema viongozi hao wa kitaifa walifanya mengi katika nchi hii kutokana na jasho lao ikiwemo kuunganisha nchi mbili kati ya Tanganyika na Zanzibar na kupata Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Waziri alisema serikali imeandaa utaratibu wa kisheria wa kuwaenzi viongozi wa kitaifa katika sheria ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2021 iliyoweka utaratibu ya wiki wa kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa na Waasisi wa Mapinduzi.

Msemaji wa Familia, Jafar Abdalla Mussa, kwa niaba ya familia, aliishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuendelea kuwakumbuka viongozi hao kwa kufanya ziara ya kuwasomea dua wazee wao .

Aidha aliiomba serikali kuwa karibu na vizazi vya marehemu hao ili kupata msaada mbali mbali unapohitajika katika familia hiyo.



# Waziri asisitiza mfumo taarifa usajili ardhi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Rahma Kassim Ali, amesema mfumo wa taarifa za usimamizi na usajili wa ardhi utasaidia kuondosha migogoro ya ardhi.

Aliyasema hayo jana baada ya kushuhudia utiaji saini hati ya makubaliano kwa wizara hiyo na Shirika la Kitaifa la Kijografia na Misitu ya Ufaransa (IGN FI) kuhusu mfumo huo uliofanyika katika ofisi za wizara hiyo, Maisara mjini Unguja.

Alisema utiaji saini huo una manufaa makubwa hasa katika kuondoa migogoro ya ardhi ambayo inajitokeza kila siku.

Waziri Rahma alibainisha kuwa hivi sasa wizara inaendelea na zoezi la utambuzi wa ardhi ambapo pia taarifa zake zitaingia katika mfumo na tayari shehia 50 zimeshafanyiwa kazi na mategemeo ya serikali ni kuitambua ardhi yote katika shehia 388.



Alisema wanaamini wakishafanya utambuzi huo na taarifa zikaingia katika mfumo asilimia 95 ya migogoro ya ardhi itaondoka. Pia alisema mfumo huo pia utasaidia kuondosha masula ya uvamizi wa ardhi.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Mngereza Mzee Miraji, alisema mfumo huo utakapoanza kazi utakuwa na faida kubwa ikiwamo kuongeza usalama wa umiliki wa ardhi kwa wawekezaji na wananchi.

Mrajis wa Ardhi, Dk. Abdul-Nasser Hikmany, alisema mfumo huo utasaidia kiutendaji pamoja na kutoa huduma bora kwa jamii.

Alisema ni malengo yao kuwa taarifa zote ambazo zitahusu ardhi zitaingizwa katika mfumo huo ikiwemo utambuzi, mipango miji, usajili na mambo mingine ikiwemo maombi.

Alibainisha kuwa mfumo huo si mgeni na umeshatumika katika nchi nyingine ikiwemo Uganda, Seralione na hata Tanzania Bara ambao hufanya kazi kwa muda wa miaka mitano.

Mkurugenzi Mkuu wa IGN FI, Christopher Dekeyne, aliipongeza serikali kufanya kazi pamoja na shirika hilo katika utekelezaji wa mfumo ambao utasaidia sana kubadili usimamizi wa ardhi hapa Zanzibar na kuahidi kufanya kazi bora.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA TRAILER

**TANGANYIKA UNIVERSAL LTD** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TRAILER** yenye usajili namba **T 705 AFY.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **TAR/RB/263/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA TRAILER

**TANGANYIKA UNIVERSAL LTD** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TRAILER** yenye usajili namba **T 882 AME.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **TAR/RB/263/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GIDEON TABANI KIBAGO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA PROBOX VAN** yenye usajili namba **T317DND.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **TAR/RB/489/2023**

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO ....06...OF 2023**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ANTONY COSMAS KAHAMBAKAMWE**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LATER OF ADMINISTRATION**
**BY JOSEPH ANTONY**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections of the grant should be filed on or before the 24 day of April 2023

Dated at korogwe this 23 day of March.

DISTRICT COURT KOROGWE

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(KIGOMA DISTRICT REGISTRY)**
**AT KIGOMA**
**(LAND DIVISION)**

**LAND CASE NO 22 OF 2022**

**PASCHAL LEONARD BILIGWA..............................1ST PLAINTIFF**

**THE REGISTERED TRUSTEES OF MHUBILI CHURCH OF GOD.........................2ND PLAINTIFF**

**VERSUS**

**TOFIKI IBRAHIM KALENGA ................................1ST DEFENDANT**
**KABANGA INVESTMENTS LIMITED ....................2ND DEFENDANT**

**NOTICE OF DATE OF HEARING**

**TO: 1. TOFIKI IBRAHIM KALENGA**
**2. KABANGA INVESTMENTS LIMITED.**

**TAKE NOTICE**

That the above named suit has been fixed for hearing on 24/4/2023 at 09:00 hours. You are hereby summoned to appear to this court in person or by advocate or any agent without fail. The hearing will proceed if you will fail to attend without any notice, and Judgment will be pronounced in your absence.

Given under my hand and the seal of this court this day 2803/2023.

AG - DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT KIGOMA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) MANYONI**

**MAOMBI NA. 18 YA 2022**

**PANDILA DILEMWA .......................................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**DAUD MISANGO ........................................MJIBU MAOMBI NA. 1**
**COSMAS LWAMBANO ............................... MJIBU MAOMBI NA. 2**
**MUSA COSMAS ....................................... MJIBU MAOMBI NA. 3**

**KWA:**
**MUSA COSMAS**
**POPOTE ULIPO TANZANIA**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala za maombi ambazo zinaweza kupatikana katika Baraza hili,

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria tarehe 12/06/2023 saa 2:30 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo na kwa kuwa ni ya kutajwa kwa shauri hilo ni lazima ulete hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIA:**
Kushindwa au kupuuza kufika terehe na saa iliyotajwa hapo juu kesi itaendelea kusikilizwa upande mmoja.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Baraza hili leo tarehe 21/03/2023

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) MANYONI

MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MANYONI TANZANIA

## UNCLE MO ENTERPRISES
## TANGAZO LA KUKUSANYA DENI

Kwa mamlaka niliyopewa na **RENATUS SIRILI KIMARIO** ninatangaza kukusanya deni linalotokana na kiwanja namba **140 KITALU "B"** Mahungu katika halmashauri ya jiji la Dodoma deni lenye thamani ya Tsh. 7,000,000/= linalotokana na kushindwa kukamilisha malipo ya ununuzi wa kiwanja tajwa hapo juu.

Mdaiwa anapewa kipindi cha miezi minne (4) tu toka tarehe ya tangazo hili na endapo atashindwa kukamilisha malipo tajwa humu ndani basi hati ya kiwanja tajwa hapo juu itarejeshwa kwa mmiliki

MORRIS NDOMBA
MKURUGENZI MTENDAJI

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MOHAMED MOHSEN AL-AMRY,** Anatangaza Kupotea kwa Kadi ya Gari aina ya **TOYOTA NOAH** Yenye no za Usajili **T637CEH,** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo Cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **DOD/CHE/RB/116339/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MASS _ UNIVESAL,** Anatangaza Kupotea kwa Kadi ya Gari aina ya **SUZUKI CARY** Yenye no za Usajili **T 131 CUE** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo Cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **DOD/CHE/RB/116317/2023.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**GODGRACE HARRY MACHA** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye namba **TAE563811** iliyotolewa makao makuu Dar es Salaam mwaka 2023. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/KIL/RB/118734/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Njombe**

**Kituo cha Njombe Mjini**
**Mkoa Njombe**

**Usimamizi wa mirathi Na. 21/2023**

**WITHO EMMANUEL MPOLO....................Marehemu**
**ASIFIWE EMMANUEL MPOLO...............Msimamizi**

**TAARIFA KWA WADAI**
**(Kanuni ya 9 (1) ya Nyongeza ya V ya Sheria ya Mahakimu kwa Mahakama Sura ya 11 Rejeo la 2019)**

TAARIFA inatolewa hapa kwa wote wanaodai kuwa na madai yanayohusiana na mali za marehemu mtajwa hapo juu WITHO EMMANUEL MPOLO, aliyefia Njombe tarehe 18 Februari 2023, na Mahakama kunipa barua ya usimamizi wa mirathi hiyo ASIFIWE EMMANUEL MPOLO siku ya tarehe 27 Marchi, 2023, hapa sasa wanatakiwa kunipa madai yao kwangu kupitia namba sanduku langu la barua............Njombe au namba ya simu 0652333955, au kuniletea kwa binafsi, ndani ya siku 10 kuanzia tarehe ya kutangazwa taarifa hii ambapo muda wake utapoisha nitaendelea kukabidhi mali za marehemu kwa warithi wanaostahili, nikizingatia tu madai ambayo nitakuwa nimearifiwa.

Imepitishwa

HAKIMU MKAZI
NJOMBE - MJINI

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MARTIN ADOLF MCHEMWA** anatangaza kupotea kwa kadi ya agri aina ya SUBARU-LEGACY yenye usajili namba T799 DGQ , CHASSIS NAMBA: BL5055716 na ENGINE NAMBA:EJ20EAA5716. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.POLISI TAARIFA: **DOD/DOD/RB/119030/2023**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**LILILOKO DODOMA**
**MAOMBI NA. 154 YA 2021**
**MICHAEL MGONGOLWA .........MDAI**
**VERSUS**
**DAMASI SILVESTER THADEI ......MDAIWA 1**
**MAKALI DANIEL .......... MDAIWA 2**

**KWA:**
**DAMASI SILVESTER THADEI**
**MAKALI DANIEL**
**POPOTE ULIPO.**
**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 11.04.2023 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

**ANGALIZO**: kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 31 ya mwezi wa MACHI, 2023.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MELKIZEDEK SARO KIKOKA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T883 AQF.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **MBE/RUJ/RB/116903/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**LEIYABU MAGOMA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1402/0055/2014** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KASAMWA SECONDARY SCHOOL** mwaka **2014.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **NZ/RB/4800/2019**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA (MCA) 63**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO IBWERA, WILAYA YA BUKOBA.**
**AJALA KOKUPIMA SAIDI .......MDAI**
**DHIDI YA**
**AMINI KANUMA SAIDI ........MDAIWA**

Amini Kanuma Saidi unatakiwa kuhudhuria katika mahakama hii tarehe 18/04/2023 saa 2:30 Asubuhi kuja kujibu madai ukiwa na shahidi wako.

Kwa kuwa ni siku ya kukata shauri fika na hati zote zinazohusiana na shauri hilo na kama hautahudhuria shauri hili litaendelea kusikilizwa upande mmoja.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Mhuri wa Mahakama hii.

C. R. RICHARD
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO IBWERA.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA KARAGWE - KAYANGA**
**MAOMBO NA. 02/2023**
**PHILEMON PHILIPO KAMPUGA .......MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**1. MARTINA PASCHAEL**
**2. AMOS ISRAEL**
**3. AMOS PHILIPO**
**4. PATRICK FRANK**
**5. ERICK PASCHAEL ..........WAJIBU MAOMBI**

**KWA: AMOS ISRAEL, PATRICK FRANK (POPOTE PALE ULIPO)**

Unaarifiwa kuwa kesi Na. 09/2023 imepangwa kutajwa tarehe 03/05/2023 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, D. S. DAVID saa 2:00 asubuhi, mahali - KAYANGA - KARAGWE.

Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasilikiliza shauri upande mmoja dhidi yako.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 31/03/2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
KAYANGA - KARAGWE

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 0677020701**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**Website: www.ippmedia.com**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Trump kuanza kibarua kipya mahakamani

**NEWYORK, Marekani**

RAIS wa zamani wa Marekani Donald Trump, amewasili katika jiji la New York ili kufunguliwa mashtaka ya jinai.

Mashtaka hayo yanatishia nafasi yake ya kugombea kiti cha urais wa Marekani katika uchaguzi wa mwaka 2024.

Trump alianza safari yake ndefu ya magari kutoka makazi yake ya mar-a-Lago yaliyoko Florida, kisha alipanda ndege yake ya kibinafsi iliyochorwa jina lake kwa maandishi ya rangi ya dhahabu.

Wakati wote huo, wafuasi wake walikuwa wakimshangilia wakilaani mashtaka dhidi yake.

Kundi dogo la wafuasi wake wengine walifanya maandamano huku wakiwa wamebeba bango lililokuwa na maandishi "Maliza Ukuta Trump24" maandishi hayo yakimaanisha Trump akamilishe azma yake ya kutaka kujenga ukuta kati ya Marekani na Mexico ili kuzuia wahamiaji haramu atakapoingia madarakani mwaka 2024.

Wakati akiwasili, hatua kadhaa za kiusalama katika mji huo zilichukuliwa na Meya wa mji huo aliwaonya wanaonuia kuleta aina yoyote ya vurugu.

Trump alitarajiwa kujisalimisha mbele ya ofisi ya mwendesha mashtaka wa Manhattan jana na alama zake za vidole zitachukuliwa kabla kufika mbele ya jaji kusomewa mashtaka ambayo atayakanusha.

Kutopeperushwa moja kwa moja

Waendesha mashtaka walisema kesi dhidi yake haina uhusiano wowote na siasa na wameitetea kazi ya mwendesha mashtaka wa Manhattan Alvin Bragg, anayeiongoza kesi hiyo.

Huku akikiongezea nguvu kikosi chake cha mawakili, duru zinaarifu Trump, amemchagua Todd Blanche kuingia katika orodha ya mawakili watakaomuwakilisha katika kesi hiyo.

Blanche ni wakili maarufu wa kesi za jinai na mwendesha mashtaka wa zamani wa shirikisho.

Blanche na mawakili wengine wa Trump walimtaka jaji katika kesi hiyo asitoe idhini ya upigaji picha, video na hata upeperushwaji wa matangazo ya moja kwa moja katika redio akifikishwa kizimbani mteja wao.

Katika barua iliyowasilishwa mahakamani, mawakili hao wamehoji kuwa kukubalia tukio hilo lipeperushwe katika vyombo vya habari, kutachochea ongezeko la mazingira mabaya ya uendeshaji wa kesi hiyo na kuondolewa heshima kikao hicho cha mahakama.

Kikosi kilichomchunguza Trump kwa miezi kadhaa mwaka huu, kilisikiliza ushahidi uliotolewa kuhusu dola 130,000 ambazo Trump anadaiwa kumlipa mwanamke mmoja mcheza filamu za ngono Stormy Daniels, katika siku za mwisho za kampeni ya mwaka 2016.

Trump aliushinda uchaguzi huo na kuwa rais wa Marekani

Daniels alisema alilipwa ili asifichue taarifa kuhusu mahusiano ya kingono aliyokuwa nayo na Trump katika hoteli moja mwaka 2006.

Trump anakanusha kuwa na uhusiano wowote na mwanamke huyo.

Baada ya kusimama kizimbani, ofisi ya Trump ilisema rais huyo wa zamani atarudi nyumbani kwake Florida na kukutana na waandishi wa habari, ili kutoa maoni kuhusu kesi hiyo.

*DW*



Ndege binafsi ya Rais wa zamani wa Marekani, Donald Trump **PICHA:MTANDAO**

# Kenya kurusha setelaiti anga za juu

**NAIROBI, Kenya**

NCHI ya Kenya inajiandaa kurusha satelaiti yake ya kwanza itakayofanya kazi ya uchunguzi wa dunia.

Hatua hiyo imetajwa kuwa ni mafanikio ya kihistoria katika juhudi za uchunguzi wa anga la juu nchini humo.

Setelaiti hiyo iliyopewa jina la 'Nation-I' au 'Taifa-' kwa Kiswahili, imeratibiwa kurushwa wiki ijayo kwa roketi ya SpaceX Falcon 9 kutoka kituo cha anga cha Vandenberg katika jimbo la California, nchini Marekani.

Wizara ya Ulinzi na Shirika la Anga la Kenya, zilisema Satelaiti hiyo imeundwa ili kutoa data ya uchunguzi wa ardhi kwa ajili ya matumizi ya kilimo, usalama wa chakula na usimamizi wa mazingira.

"Iliundwa kikamilifu na kuendelezwa na wahandisi wa Kenya kwa ushirikiano na mtengenezaji wa anga ya Bulgaria," taarifa hiyo iliongeza.

Ujumbe kutoka Kenya unatarajiwa kusafiri kwenda Marekani kwa ajili ya uzinduzi huo.

Misheni hiyo inaonekana kama hatua muhimu kwa uvumbuzi wa kisayansi wa Kenya.

Nchi hiyo inakabiliwa na ukame mbaya zaidi kuwahi kutokea katika miongo kadhaa baada ya misimu mitano ya mvua kutonyesha.

Mnamo 2018, Kenya ilizindua majaribio yake ya kwanza ya satelaiti ya tano kutoka Kituo cha Kimataifa cha Anga za Juu.

*BBC*

## Nasa kumpeleka mtu mweusi angani kuzunguka mwezi

**WASHINGTON, Marekani**

SHIRIKA la anga za juu la Marekani (Nasa), limewataja wanaanga wanne ambao watakwenda kuzunguka mwezi, baada ya kufanya hivyo miaka 50 iliyopita.

Hata hivyo, jina la Christina Koch, limeibua mjadala baada ya kuwa mwanaanga mwanamke wa kwanza kuwahi kutumwa kwenye mwezi, huku Victor Glover akiwa mwanaanga wa kwanza mweusi.

Wanaanga hao wataungana na Reid Wiseman na Jeremy Hansen kuendesha chombo kuzunguka Mwezi mwishoni mwa mwaka ujao au mapema mwaka wa 2025.

Wanaanga hawatatua Mwezini, lakini misheni yao itafungua njia ya kuwapeleka wafanyakazi wengine.

Raia hao watatu wa Marekani na Canada, waliwasilishwa kwa umma katika hafla iliyofanyika mjini Houston, Texas.

Kuanzia sasa wataanza kipindi cha mazoezi makali ili kujiweka tayari.

Katika kuchagua mwanamke na mtu wa rangi, Nasa inatimiza ahadi yake ya kuleta utofauti mkubwa katika juhudi zake za uchunguzi.

Misheni zote za hapo awali za wafanyakazi kwenda Mwezini zilifanywa na wazungu.

Reid Wiseman (47)ni rubani wa Jeshi la Wanamaji la Marekani ambaye alihudumu kwa muda kama mkuu wa ofisi ya mwanaanga ya Nasa.

Aliendesha safari moja ya awali ya kwenye anga, hadi kituo cha anga za juu cha Kimataifa mwaka wa 2015.

Victor Glover (46) ambaye ni rubani wa majaribio ya Jeshi la Wanamaji la Marekani, alijiunga na Nasa mwaka 2013 na kufanya safari yake ya kwanza ya anga mnamo 2020. Alikuwa Mwafrika wa kwanza kukaa kwenye kituo cha anga za juu kwa muda mrefu wa miezi sita.

Christina Koch (44) ni mhandisi wa umeme, anashikilia rekodi ya muda mrefu zaidi angani kwa wanawake, ya siku 328.

Akiwa na mwanaanga wa Nasa, Jessica Meir alishiriki katika matembezi ya kwanza ya anga ya juu wote wakiwa wamawake mnamo Oktoba 2019.

Jeremy Hansen (47), kabla ya kujiunga na Shirika la Anga za Juu la Canada, alikuwa rubani wa kivita katika Jeshi la Wanahewa la Canada.

Bado hajawahi kwenda kwenye anga.

*BBC*

# SIMBA QUEENS, FOUNTAIN GATE PRINCESS KUTIFUANA LEO DODOMA

**Na Adam Fungamwango**

MACHO na masikio ya mashabiki wa soka la wanawake, leo yataelekezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma wakati Mabingwa Watetezi, Simba Queens, watakapokuwa wageni wa timu machachari ya Fountain Gate Princess, ikiwa ni raundi ya 13 ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Wengi wanaitazama kuwa ni mechi ambayo huenda inaweza kutoa bingwa wa Tanzania Bara msimu huu kutokana na timu hizo kufukuzana kwa karibu kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Fountain Gate Princess inayoongoza ligi hiyo ikiwa na pointi 29, inahitaji ushindi ili iweze kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kuipokonya Simba Queens ubingwa kwani itafikisha jumla ya alama 32 na kuwaacha mabingwa hao na pointi zao 28.

Endapo Simba Queens inayokamata nafasi ya pili itashinda itakuwa na pointi 31, na kuizidi Fountain Gate Princess kwa pointi mbili, ikirejea tena kileleni.

Mashabiki wengi wanaichukulia mechi hiyo kama fainali kwani wanaona baada ya hapo, timu hizo hazitokuwa na upinzani mkubwa sana kwenye mechi zingine zitakazofuata za ligi hiyo.

Mechi zote za raundi ya 13 zitachezwa leo ambapo mbali na mechi hiyo, The Tigers Queens itakuwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid dhidi ya Baobab Queens, Amani Queens itakuwa nyumbani Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi kucheza dhidi ya Mkwawa Queens, katika Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza, Alliance itaialika Yanga Princess na JKT Queens itakuwa Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Mbweni nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam kucheza dhidi ya Ceasiaa Queens.



Winga wa Mtibwa Sugar, Ladack Chasambi, akipiga hesabu ya kuwahadaa wachezaji wa Azam FC, mshambuliaji Prince Dube (kushoto) na kiungo James Akaminko, katika mechi ya robo fainali ya Kombe la FA, iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi juzi na kumalizika kwa wenyeji kushinda mabao 2-0. **HABARI UK. 23. MPIGAPICHA WETU**

# Aziz Ki, Morrison 'fiti' kuivaa Geita Gold

**Na Saada Akida**

NYOTA wawili wa Yanga, Stephane Aziz Ki, na Bernard Morrison, wamereje uwanjani na wako fiti kwa mechi zilizopo mbele yao ikiwamo Kombe la Shirikisho la Azam dhidi ya Geita Gold FC.

Katika mchezo huo wa robo fainali, Yanga watawakaribisha Geita Gold FC, Jumamosi wiki hii kwenye Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam.

Akizungumza na gazet hili jana, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, alisema nyota hao walikuwa majeruhi na sasa wamerejea na wataonekana katima michezo ijayo ukiwamo dhidi Geita Gold FC.

Alisema Aziz Ki aliumia na hakucheza mechi dhidi ya TP Mazembe na amerejea sambamba na Morrison, ambao watakuwa katika mipango ya mchezo huo ujao wa Kombe la Shirikisho.

"Tunatambua Geita Gold FC ni timu nzuri, mara ya mwisho tuliwafunga katika ligi kwenye uwanja ambao tunaenda kucheza nao hivi karibuni, tunatarajia kuwapo na mabadiliko ndani ya kikosi kwa kuwapumzisha baadhi ya wachezaji," alisema Kaze.

Aliongeza kuwa mchezo huo utakuwa mgumu kulingana na wapinzani hao wataingia na mbinu zingine kwa kuwa mechi ya iliyopita ya Ligi Kuu dhidi yao walipoteza.

"Hii ni mechi muhimu, lazima utafute ushindi ili kutete taji, tuna waheshimu wapinzani kwa sababu safari hii hawatakuja kama ilivyokuwa mechi ya ligi ambayo tuliwafunga," alisema kocha huyo. Alisema baada ya mapumziko ya siku tatu, kesho (Alhamisi) wanaingia kambini kujiandaa na mchezo huo, lakini pia kuutumia kama maandalizi ya kuwakabili Simba Aprili 16, mwaka huu.

## Mwarabu alamba mil. 54/- Meridianbet

**Na Saada Akida**

MKUU wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano wa Kampuni wa mchezo wa Kubashiri Meridianbet, Matina Nkurlu, amemtangaza mshindi wa Sloti ya 100 Burning Hot, Saleh Mwarabu, ambaye amejinyakulia kitita cha Sh. 54,700,000.

Akizungumza na gazeti hili jana, Matina alisema Mwarabu amejinyakulia mamilioni hayo kutoka Meridianbet baada ya kucheza moja ya sloti pendwa kabisa ya kasino ya mtandaoni na kuweka dau lake dogo.

"Gwiji huyu ni mkazi wa Dar es Salaam alicheza Slot ya 100 Burning Hot, inayopatikana kwenye kasino ya mtandaoni ya Meridianbet, Slot hii inalipa sana kwani ushindi ni rahisi kuupata kwa dau dogo tu kuanzia Sh. 100," alisema Matina na kuongeza kuwa Mwarabu alishinda kwa dau dogo la 50,000 kupitia kasino ya mtandaoni.

Matina alisema Sloti ya 100 Burning Hot, ni miongoni mwa michezo pendwa ya kasino inayotoa mkwanja muda wowote, pia Sloti nyingine rahisi kushinda ni Aviator, Poker na Titan Roulette zote unazipata kwenye kasino ya mtandaoni ya Meridianbet.

## KMKM hakuna kulala mbio ubingwa Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya KMKM imesema malengo yao makubwa ni kuhakikisha wanaweka historia ya kuchukua ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar kwa misimu mitatu mfululizo.

KMKM ndio vinara wa Ligi Kuu Zanzibar wakiwa na alama 54 wakipishana alama moja na wapinzani wao KVZ wenye alama 53.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa KMKM, Ame Msimu, alisema licha ya ligi kusimama kwa ajili ya kupisha mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, lakini timu hiyo inatarajia kuendelea na mazoezi yake wiki ijayo.

Alisema wachezaji ambao wapo nje ya Zanzibar wataanza kuwasili kambini mwishoni mwa wiki hii ili kujiandaa na michezo mitano ya ligi iliyobakia wakilenga kutimiza lengo lao la kutetea ubingwa wao.

"Mipango yetu inaendelea bado kama tulivyoanza nayo ya kuhakikisha tunanyakuwa ubingwa msimu huu ili kutufanya tuweze kuubeba mara tatu mfululizo, hili hakika tutafanikiwa licha ya kupishana alama ndogo na mpinzani wetu," alisema.

## ZISIKUPITE

### POTTER AIKATALIA LEICESTER
GRAHAM Potter amekataa fursa ya kuchukua usukani kama kocha wa Leicester baada ya kutimuliwa Chelsea. ***(Talksport)***

### ENRIQUE ATAJWA CHELSEA
KOCHA wa zamani wa Barcelona na Hispania, Luis Enrique, ameibuka kama mtu anayeweza kuwa kocha mpya wa Chelsea. ***(Sun)***

### TIELEMANS ATAKIWA ARSENAL
KLABU ya Arsenal imefanya mazungumzo na kiungo wa kati wa Ubelgiji, Youri Tielemans, mwenye umri wa miaka 25, ambaye mkataba wake na Leicester City unakamilika msimu huu. ***(TeamTalk)***

### MAKOCHA WATANO CHELSEA
CHELSEA inataka kuwahoji makocha watano kuhusu nafasi yao iliyo wazi, wakiwamo Luis Enrique, Julian Nagelsmann, Mauricio Pochettino, Luciano Spalletti wa Napoli na mwingine mmoja. ***(Telegraph)***

### KANE AWANIWA UNITED
KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, anaona nahodha wa England, Harry Kane kama chaguo lake la kwanza la mshambuliaji msimu huu, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, yuko tayari kusaini mkataba mpya Tottenham. ***(Athletic)***

### AMORIM, GLASNER NAO PIA
KOCHA wa Sporting Lisbon, Ruben Amorim na bosi wa Eintracht Frankfurt, Oliver Glasner, pia wanawaniwa Chelsea. (***Guardian)***

### NAGELSMANN TATIZO UMRI
UONGOZI wa Chelsea una wasiwasi kuhusu umri wa kocha zamani wa Bayern Munich Nagelsmann, 35. ***(Sky Sports)***

### MAGUIRE KUPELEKWA SOKONI
MLINZI wa England, Harry Maguire, mwenye umri wa miaka 30, atauzwa Manchester United mwishoni mwa msimu huu. ***(Manchester Evening News)***

### PAVARD AZIDI KUWINDWA
KLABU ya Manchester United imefanya mazungumzo ya kiuchunguzi kuhusu kumsajili beki wa pembeni wa Ufaransa, Benjamin Pavard mwenye umri wa miaka 27, kutoka Bayern Munich. ***(Athletic)***

### FRIMPONG KUNG'OLEWA LEVERKUSEN
MANCHESTER United imeanza mazungumzo juu ya kumsajili beki wa pembeni wa Bayer Leverkusen na Uholanzi, Jeremie Frimpong mwenye umri wa miaka 22. ***(Florian Plettenberg)***

### SPURS INAMTAKA RODGERS
KLABU ya Tottenham Hotspur inamtaka Brendan Rodgers kuwa kocha wao mpya baada ya kutimuliwa kule Leicester City. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KLOPP: MIMI SIOGOPI KUFUFUKUZWA LIVERPOOL

Ninafahamu ukweli kwamba nimeketi hapa kwa sababu ya tulichofanya siku za nyuma, wamiliki wanajua kuhusu...

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp amesema "haogopi" kutimuliwa na Liverpool wakati wa msimu mbaya wa klabu hiyo na hasa baada ya kufukuzwa kwa makocha wengi kwenye Ligi Kuu England.

Klabu hiyo ya Merseyside imeporomoka hadi nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu baada ya kupokea kichapo cha tatu mfululizo kwa kuchapwa mabao 4-1 na Manchester City Jumamosi.

Kikosi cha Klopp pia kilitolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Real Madrid katika hatua ya 16-bora mwezi uliopita.

Baada ya kuondoka kwa Kocha wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte, Graham Potter katika klabu ya Chelsea na Brendan Rodgers Klabu ya Leicester City, Klopp alisema hakuna haja ya kuogopa kuondolewa kwenye wadhifa wake, lakini akakiri kuwa timu yake imeshuka chini ya viwango vyao msimu huu.

"Ninafahamu ukweli kwamba nimeketi hapa kwa sababu ya siku za nyuma, si kwa sababu ya kile tulichofanya msimu huu," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Tuna wamiliki mahiri -- wanajua kuhusu hali hiyo. Ikiwa huu ulikuwa msimu wangu wa kwanza, ingekuwa tofauti kidogo.

"Siogopi. Hakuna haja ya kuogopa, ninahitaji kutoa. Siko hapa kama mchoro wa ukuta kwenye kuta za nyumba, niko hapa kutoa.

"Niko ndani kabisa - lakini inabidi tulitatue hili. Hatuwezi kuendelea tu kucheza jinsi tunavyocheza mara kwa mara. Nimesikitishwa sana na sisi kwamba tunafanya hivi, lakini hutokea. Lazima tutafute njia ya kutokea."

Kuondoka kwa Potter, Conte na Rodgers kulimaanisha kuwa makocha 12 wamefukuzwa kazi katika Ligi Kuu England msimu huu.

Klopp alisema idadi ya makocha waliofukuzwa ni "mbaya", lakini akaongeza kuwa "ni sehemu ya biashara."

"Nadhani klabu zote mbili haziko katika maeneo wanayotarajia kuwa," alisema. "Siwezi kusema mengi zaidi kuhusu hilo. Tuseme ninawafahamu vizuri, nawaheshimu sana.

"Nilipokutana nao walikuwa watu wazuri sana na wasimamizi wazuri sana wote wawili. Lakini bado mambo yanaweza kwenda ndivyo sivyo na kisha watoa maamuzi kwenye klabu wanadhani lazima wabadilike na wakabadilika."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,099,1

JACKPOT
MECHI WIKI HII
TAREHE: 05,06 NA 07 APRILI 2023
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 05/04/23 | 21:15 | Perugia vs Reggina | 2.52 | 2.94 | 2.83 |
| 02. 05/04/23 | 21:45 | RB Leipzig vs Borussia Dortmund | 2.29 | 3.60 | 2.90 |
| 03. 05/04/23 | 22:00 | Barcelona vs Real Madrid | 2.29 | 3.21 | 2.96 |
| 04. 05/04/23 | 22:00 | West Ham vs Newcastle | 3.00 | 3.25 | 2.22 |
| 05. 06/04/23 | 01:00 | Danubio FC vs SC Emelec | 2.38 | 3.05 | 2.84 |
| 06. 06/04/23 | 02:00 | Huachipato vs Union Espanola | 2.40 | 3.21 | 2.69 |
| 07. 06/04/23 | 04:05 | Pumas De Tabasco vs Zacatepec | 2.89 | 3.36 | 2.19 |
| 08. 06/04/23 | 05:00 | Deportivo Pereira vs Colo Colo | 2.58 | 3.08 | 2.58 |
| 09. 06/04/23 | 19:00 | Slask Wroclaw vs GKS Piast Gliwice | 2.43 | 3.09 | 2.67 |
| 10. 06/04/23 | 22:15 | El Ittihad Alexandria vs Coca Cola | 2.86 | 2.91 | 2.56 |
| 11. 07/04/23 | 03:00 | FBC Melgar vs Olimpia Asuncion | 2.25 | 3.13 | 2.98 |
| 12. 07/04/23 | 03:00 | CA Tigre vs Sao Paulo | 2.54 | 3.06 | 2.64 |
| 13. 07/04/23 | 08:00 | Western United vs Central Coast Mariners | 2.68 | 3.26 | 2.47 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# RAIS WA UEFA ATOA NENO KASHFA WAAMUZI BARCA



**NYON, Uswisi**

RAIS wa Shirikisho la Vyama vya Soka Ulaya (Uefa), Aleksander Ceferin, amesema kashfa ya waamuzi inayoikabili Barcelona ni moja ya hali mbaya zaidi ambayo amewahi kuona katika soka.

Shirikisho la Soka barani Ulaya lilitangaza Machi kuwa lilifungua uchunguzi kuhusu malipo ambayo Barca ilitoa kwa makamu wa rais wa zamani wa kamati ya waamuzi ya Hispania.

Kuanzia mwaka 2001 hadi 2018, Barca ililipa zaidi ya euro milioni saba kwa Jose Maria Enriquez Negreira.

Klabu hiyo ya Katalunya imesema walikuwa wakinunua "ripoti za kiufundi kuhusu waamuzi" na wanakana kuwahi kununua maafisa wa mechi au ushawishi.

"Hali ni mbaya sana," alisema Ceferin katika mahojiano na gazeti la nchini Slovenia, Ekipa, Jumatatu alipoulizwa kuhusu matukio yanayoizunguka Barca.

"Ni mbaya sana, kwa maoni yangu ni moja ya hali mbaya zaidi katika soka ambayo nimewahi kuona," alisema.

Waendesha mashtaka wanafuatilia mashtaka dhidi ya Barca kwa madai ya rushwa, huku mahakama nchini Hispania ikikubali kufungua uchunguzi kuhusu klabu hiyo na marais wa zamani, Sandro Rosell na Josep Maria Bartomeu.

Real Madrid na mashirika kadhaa ya michezo nchini humo pia yamejiunga na kesi ya waendesha mashtaka.

Rais wa LaLiga, Javier Tebas ameitaja kashfa hiyo kuwa "mgogoro mbaya zaidi wa sifa" anaoweza kuukumbuka katika soka la Hispania na kumtaka rais wa Barca, Joan Laporta kufuta malipo hayo.

Laporta alisema anapanga kufanya mkutano na wanahabari mara tu uchunguzi wa ndani utakapokamilika.

Lakini Tebas pia amethibitisha LaLiga haitaweza kuiadhibu Barca kwa sababu ya sheria ya mapungufu ya nchini Hispania -- ingawa Ceferin alifichua Uefa haikabiliwi na vikwazo kama hivyo.

"Siwezi kutoa maoni moja kwa moja juu ya hili kwa sababu mbili," alisema Ceferin.

"Kwanza kwa sababu tuna kamati huru ya nidhamu inayosimamia hili, na pili, kwa sababu sijashughulikia suala hili kwa undani.

"Katika kiwango cha LaLiga, bila shaka, suala hilo limezuiliwa kwa muda na haliwezi kuwa na matokeo ya ushindani, lakini kesi zinaendelea katika ngazi ya waendesha mashtaka. Lakini kuhusu Uefa, hakuna kitu kilichozuiliwa na muda."

# Neville: United ilimkosea Ten Hag

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United haikutoa ushirikiano kwa kocha Erik ten Hag katika dirisha la usajili la Januari kwa kutomsajili mshambuliaji, nyota wa zamani wa klabu hiyo, Gary Neville amesema.

Kichapo kutoka kwa Newcastle United Jumapili kiliifanya United kushuka hadi nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, pointi moja juu ya Tottenham, ambao wanamchezo mchezo mmoja mkononi.

Kiwango cha United cha ugenini kimekuwa suala kubwa msimu huu, huku vipigo sita kati ya saba vikiwa vya ugenini, na safari zijazo itawakabili Tottenham na Brighton na Hove Albion.

Kwa mujibu wa Neville, kushindwa kwa klabu hiyo kusajili ipasavyo fowadi mpya katika dirisha la katikati ya msimu, baada ya kuondoka kwa Cristiano Ronaldo, ndio chanzo cha matatizo yao.

"Hakupewa ushirikiano Erik ten Hag Januari. Kwa sababu mahojiano hayo ya Cristiano Ronaldo na Piers Morgan yalifanyika Novemba," alisema.

"Manchester United basi walikuwa na wiki sita kabla ya dirisha la uhamisho kuanza. "Walifanya uamuzi wa kutompa Erik ten Hag fedha hizo za usajili. Walifanya uamuzi wa kumwambia kwamba atalazimika kuleta mtu kwa mkopo.

"Nani ataipa Manchester United kwa mkopo mshambuliaji wa kiwango cha kimataifa Januari? Hakuna mtu atafanya hivyo. "Simlaumu Wout Weghorst hata kidogo. Amefanya kazi nzuri sana. Yeye ni mshika nafasi wa Manchester United na Erik ten Hag, na nadhani anafanya kila kitu anachoweza kufanya pale.

"Ni wazi hafai kuwa mshambuliaji wa Manchester United. Lakini walihitaji kuungwa mkono Januari.

"Walimpoteza Ronaldo, walimpoteza Edinson Cavani majira ya joto, na Anthony Martial alikuwa majeruhi. Huwezi kucheza bila mshambuliaji wa kati. Ili kucheza mpira vizuri mshambuliaji wako wa kati na kipa wako lazima acheze vizuri.

164,188/-

# AZAM TUNAMTAKA YEYOTE NUSU FAINALI FA- ONGALLA

**Adam Fungamwango na Shufaa Lymo**



BAADA ya kufanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), maarufu Kombe la FA, Azam FC imetamba kuwa itacheza na timu yoyote ile itakayokuja mbele yao na watafanya kweli kama walivyofanya kwenye mechi zote za michuano hiyo waliyocheza.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Kalimangonga Ongalla, amesema kuwa baada ya mechi hiyo wanakwenda kuangalia mapungufu machache aliyoayaona na timu yake ipo tayari kucheza na timu yoyote ile na kuwaahidi mashabiki wa Azam FC kuwa watamaliza kama walivyoanza.

Alisema hayo baada ya kuifunga Mtibwa Sugar mabao 2-0 juzi kwenye Uwanja wa Azam Complex, mechi ya robo fainali ya Kombe la FA, ikiifuata Singida Big Stars ambayo nayo imetinga hatua hiyo kwa kuibamiza Mbeya City mabao 4-1 Jumapili iliyopita.

"Kikubwa ni kwamba tumeweza kuendelea kwenye mashindano, kipindi cha kwanza kikosi hakikuwa kwenye kiwango kizuri, tuliwaacha Mtibwa waingie kwenye mchezo, lakini baadaye tumeweza kupambana na tulistahili kushinda na tulipata bao wakati sahihi, likatupa morali.

"Nawapongeza wachezaji wangu kwa kuweza muimiliki mechi licha ya kwamba tulikuwa pungufu, tunaelekea kwenye mechi nyingine lazima tuangalie mapungufu na mazuri yetu, hatuchagui timu, tutatecheza na yoyote ile, naahidi tutamaliza kama tulivyoanza," alisema Kally.

Naye Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Salum Mayanga alisema kupoteza nafasi ndiko kulikowahukumu.

"Tumeweza kucheza vizuri lakini tumepoteza, nikiri tumefanya makosa wenzetu wameyatumia. Baada ya kupoteza nafasi, wao walipopata wakaitumia, walipoteza mchezaji mmoja, kipindi cha pili tulielekezana nini tufanye, lakini wenzetu walivyorudi wakapaki basi, kikubwa ni kwamba kilichotuumiza ni kupoteza nafasi, hiyo imetugharimu na hatukuitumia nafasi ya wao kuwa pungufu.

Mabao ya washindi yalifungwa na Kipre Junior na Abdul Suleiman Sopu, huku Daniel Amoah akionyeshwa kadi nyekundu.

Kwa matokeo hayo, sasa Azam FC itakutana na mshindi wa mechi kati Simba na Ihefu FC kucheza nusu fainali, wakati Singida Big Stars ambayo Jumapili ilifanikiwa kusonga mbeke baada ya kuitandika Mbeya City kwa mabao 4-0, yenyewe itasubiri timu itakayofuzu hatua hiyo kati ya Yanga na Geita Gold FC.

# SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

## BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 08/04/23 | 17:00 | Fulham FC vs West Ham United | 2.55 | 3.15 | 2.60 |
| 02. 08/04/23 | 17:30 | Sampdoria Genoa vs US Cremonese | 2.24 | 3.10 | 3.10 |
| 03. 08/04/23 | 19:30 | Hellas Verona vs Sassuolo Calcio | 2.50 | 3.10 | 2.70 |
| 04. 08/04/23 | 19:30 | Torino FC vs AS Roma | 3.15 | 2.95 | 2.31 |
| 05. 08/04/23 | 21:45 | Lazio Rome vs Juventus Turin | 2.60 | 2.90 | 2.80 |
| 06. 08/04/23 | 21:45 | KAA Gent vs Union Saint-Gilloise | 2.46 | 3.35 | 2.60 |
| 07. 09/04/23 | 14:00 | Olympique Lyon vs Stade Rennes | 2.25 | 3.30 | 2.90 |
| 08. 09/04/23 | 15:00 | Real Valladolid vs RCD Mallorca | 2.47 | 2.90 | 2.95 |
| 09. 09/04/23 | 15:30 | FC Emmen vs NEC Nijmegen | 2.80 | 3.30 | 2.35 |
| 10. 09/04/23 | 16:00 | AC Ajaccio vs AJ Auxerre | 2.70 | 2.90 | 2.65 |
| 11. 09/04/23 | 16:00 | Montpellier HSC vs Toulouse FC | 2.28 | 3.40 | 2.80 |
| 12. 09/04/23 | 16:00 | ESTAC Troyes vs Clermont Foot 63 | 2.55 | 3.20 | 2.60 |
| 13. 09/04/23 | 16:30 | Borussia Monchengladbach vs VfL Wolfsburg | 2.26 | 3.50 | 2.75 |
| 14. 09/04/23 | 18:30 | Liverpool FC vs Arsenal FC | 2.46 | 3.45 | 2.55 |
| 15. 09/04/23 | 18:30 | VfL Bochum vs VfB Stuttgart | 2.85 | 3.20 | 2.34 |
| 16. 09/04/23 | 19:30 | UD Almeria vs Valencia CF | 2.75 | 3.15 | 2.43 |
| 17. 09/04/23 | 19:30 | Standard Liege vs KRC Genk | 2.70 | 3.45 | 2.32 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATANO - 05/04/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2404 | Kashima Antlers vs Avispa Fukuoka | 1.85 | 3.21 | 4.04 |
| 13:00 | 3207 | Jubilo Iwata vs Sagan Tosu | 3.02 | 3.17 | 2.21 |
| 13:00 | 3659 | Niigata Albirex vs Kashiwa Reysol | 2.37 | 3.11 | 2.80 |
| 13:00 | 5197 | Gamba Osaka vs FC Tokyo | 3.00 | 3.11 | 2.25 |
| 13:00 | 5398 | Shonan Bellmare vs Shimizu S Pulse | 1.90 | 3.37 | 3.63 |
| 13:00 | 5475 | Yokohama F Marinos vs Consadole Sapporo | 1.70 | 3.73 | 4.10 |
| 13:00 | 5795 | Vissel Kobe vs Sanfrecce Hiroshima | 2.57 | 3.21 | 2.50 |
| 13:30 | 3728 | Nagoya Grampus vs Yokohama | 1.52 | 3.78 | 5.59 |
| 16:15 | 2440 | Kuching FA vs Kelantan United FC | 2.13 | 3.34 | 2.93 |
| 16:30 | 2124 | Bhayangkara Surabaya Utd vs Barito Putera | 1.98 | 3.45 | 3.19 |
| 16:30 | 3371 | Persebaya Surabaya vs Persija Jakarta | 2.21 | 3.29 | 2.83 |
| 17:00 | 1447 | FK Loznica vs FK Zlatibor | 2.06 | 2.99 | 3.45 |
| 17:00 | 1532 | FK Radnicki Beograd vs Sloboda | 1.73 | 3.24 | 4.52 |
| 17:00 | 2474 | FC Rad vs FK Zeleznicar Pancevo | 3.70 | 3.08 | 1.94 |
| 17:00 | 2703 | Kedah vs Penang | 1.45 | 4.29 | 5.32 |
| 17:00 | 3589 | Kuala Lumpur vs Sabah | 2.50 | 3.19 | 2.52 |
| 17:00 | 4130 | OFK Vrsac vs FK Imt Novi Beograd | 3.49 | 3.13 | 1.98 |
| 17:00 | 4564 | Pdrm vs Pahang FA | 3.08 | 3.39 | 2.04 |
| 17:00 | 5599 | NK Aluminij vs Luka Koper | 3.51 | 3.46 | 1.90 |
| 18:00 | 1113 | Seinajoen JK vs Haka | 2.20 | 3.19 | 2.93 |
| 18:00 | 1266 | VPS Vaasa vs Lahti | 2.01 | 3.29 | 3.24 |
| 18:00 | 2630 | KuPS Kuopio vs Inter Turku | 1.88 | 3.24 | 3.70 |
| 18:00 | 3971 | Zalgiris Kaunas vs Dziugas | 1.36 | 4.40 | 6.75 |
| 18:00 | 4953 | IFK Mariehamn vs Ilves Tampere | 2.46 | 3.34 | 2.47 |
| 18:00 | 5231 | FC KTP vs AC Oulu | 2.62 | 3.29 | 2.35 |
| 18:15 | 1998 | HJK Helsinki vs Honka | 1.73 | 3.39 | 4.21 |
| 18:30 | 3665 | HNK Sibenik vs Dinamo Zagreb | 6.20 | 4.13 | 1.44 |
| 19:00 | 1307 | Nordsjalland vs Aarhus Fremad | 1.14 | 6.44 | 14.53 |
| 19:00 | 1676 | Hermanstadt vs Universitatea Cluj | 2.40 | 2.85 | 3.01 |
| 19:00 | 1789 | Olympiakos Nicosia vs AEL Limassol | 3.27 | 2.96 | 2.19 |
| 19:00 | 3619 | Nurnberg vs Stuttgart | 4.85 | 3.56 | 1.75 |
| 19:00 | 5021 | Sparta Prague vs Ceske Budejovice | 1.19 | 6.22 | 9.95 |
| 19:30 | 2309 | CSKA Moscow vs Kryliya Sovetov | 1.70 | 3.77 | 4.08 |
| 20:30 | 5616 | Galatasaray vs Basaksehir | 1.69 | 3.68 | 4.25 |
| 21:00 | 5575 | Budafoki Mte vs Vasas SC | 4.54 | 3.51 | 1.68 |
| 21:15 | 1400 | Slavia Prague vs Bohemians | 1.45 | 4.34 | 5.58 |
| 21:15 | 2553 | Servette Geneva vs FC Lugano | 2.04 | 3.39 | 3.08 |
| 21:15 | 2800 | Perugia vs Reggina | 2.16 | 3.14 | 3.25 |
| 21:15 | 3062 | Maribor vs ND Primorje | 1.30 | 4.76 | 8.08 |
| 21:30 | 1954 | Rapid Vienna vs Josko Ried | 1.46 | 4.10 | 5.81 |
| 21:30 | 5529 | Gornik Leczna vs Rakow Czestochowa | 9.32 | 4.97 | 1.26 |
| 21:45 | 5419 | RB Leipzig vs Borussia Dortmund | 2.27 | 3.65 | 2.90 |
| 22:00 | 2241 | Cremonese vs Fiorentina | 4.35 | 3.56 | 1.77 |
| 22:00 | 2639 | Barcelona vs Real Madrid | 2.36 | 3.19 | 2.87 |
| 22:00 | 3436 | West Ham vs Newcastle | 3.21 | 3.31 | 2.10 |
| 22:00 | 4147 | Manchester Utd vs Brentford | 1.66 | 3.77 | 4.49 |
| 22:10 | 5075 | Nantes vs Lyon | 3.44 | 3.44 | 2.02 |
| 22:15 | 2498 | Arab Contractors vs Pyramids | 4.21 | 3.11 | 1.90 |
| 22:15 | 3426 | Al Ahly Cairo vs Ghazl EL Mahallah | 1.25 | 5.19 | 10.98 |
| 22:15 | 5658 | Gil Vicente vs Sporting Lisbon | 6.02 | 4.32 | 1.46 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Mayele: Nina deni la kutetema Simba

INATOKA UK. 24

dhidi ya Geita Gold ikiwa na nia ya kupata ushindi ili kuendelea katika mbio za kutetea taji hilo la FA na endapo itashinda itakutana na Singida Big Stars katika hatua ya nusu fainali.

Kwa upande wa Ligi Kuu Bara, Yanga ambayo ni mabingwa watetezi, wapo kileleni wakiwa na alama 65, nane zaidi ya Simba inayoshika nafasi ya pili wakati huu timu hizo kila moja ikiwa tayari imeshuka dimbani mara 24.

# Simba yafunguka maficho ya Mkude

INATOKA UK. 24

Mkude.

Mkude, ambaye ndiye mchezaji wa muda mrefu aliyebaki kwenye timu hiyo, ni zao la kikosi cha pili cha Simba, na alipandishwa kikosi cha kwanza msimu wa 2011/12.

Michezo
Jumatano Aprili 5, 2023
Nipashe



UKURASA 21

Klopp: Siogopi kufukuzwa Liverpool

# MAYELE: NINA DENI LA KUTETEMA SIMBA SC

Aweka kando mechi ya FA Cup, asema lengo ni kumaliza msimu akiwa ameifunga...

**Na Shufaa Lyimo**

LICHA ya Yanga Jumamosi wiki hii kukabiliwa na mechi ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho la Soka la Azam (ASFC), maarufu Kombe la FA dhidi ya Geita Gold FC, mshambuliaji na kinara wa mabao wa timu hiyo, Fiston Mayele, amesema akili na hesabu zake ni kutetema dhidi ya Simba Aprili 16, mwaka huu.

Mayele ambaye mchezo uliopita wa Ligi Kuu raundi ya kwanza dhidi ya Simba alishindwa kuziona nyavu, hivyo kukosa fursa ya kushangilia kwa staili yake ya kutetema, amesema mchezo wao dhidi ya Simba utakuwa mgumu jambo ambalo linamfanya kuwa na kazi ya ziada ya ili kutimiza azma yake hiyo.

Akizungumza jijini Darnes Salaam juzi, alisema kwa sasa anauwazia mchezo huo licha ya kwamba mechi iliyopo mbele yao ni dhidi ya Geita Gold kwenye Kombe la FA na kisha Kagera Sugar katika mechi ya Ligi Kuu kabla ya kuivaa Simba.

Baada ya mchezo huo dhidi ya Geita Gold, Yanga itashuka tena Uwanja wa Azam Complex Jumanne ya wiki ijayo kuikaribisha Kagera Sugar kwenye mechi ya Ligi Kuu kabla ya Aprili 16, mwaka huu kuifuata Simba katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Katika mchezo uliopita wa ligi hiyo, timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1 shukrani kwa wafungaji Agustine Okrah aliyeitanguliza Simba kabla ya Stephano Aziz Ki kuisawazishia Yanga.

Hivyo, Mayele amesema mikakati yake ni kutetema katika mchezo huo ili atimize malengo yake ya kumaliza msimu huu akiwa ameifunga Simba.

"Mchezo wa Simba na Yanga huwa mgumu, nitahakikisha napambana kuipa ushindi timu yangu kwenye mchezo huo nikishirikiana na wachezaji wenzangu.

"Ninataka nimalize msimu huu nikiwa nimeifunga Simba, naamini hakuna kitakachoshindikana ukiwa na malengo," alisema Mayele.

Alisema anashukuru ushirikiano wanaopewa na mashabiki wao kwenye kila mchezo wanaoucheza ukiwamo ule wa Kombe la Shirikisho Afrika uliomalizika hivi karibuni dhidi ya TP Mazembe, Lubumbashi nchini DR Congo.

Mayele alisema wanaingia kambini kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wao wa Kombe la Shirikisho dhidi ya Geita Gold, watakaoucheza Jumamosi, ukifuatiwa na wa Ligi Kuu ambao watakutana na Kagera Sugar Aprili 11,kabla ya kukutana na watani wao, Simba.

Yanga itashuka dimbani

INAENDELEA UK. 23




Mayelew

## Simba yafunguka maficho ya Mkude

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Simba kimeingia kambini jana jioni kujiandaa na mechi ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC), maarufu FA Cup dhidi ya Ihefu keshokutwa, Ijumaa huku ikijibu maswali ya mashabiki wa soka kuhusu alipo kiungo mkabaji wa siku nyingi wa timu hiyo, Jonas Mkude.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema mara baada ya kurejea nchini wachezaji walipata mapumziko na waliingia kambini jana jioni tayari kwa mchezo huo unaosubiriwa kwa hamu na wapenzi wengi wa soka.

"Timu inarejea kambini kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Kombe la FA dhidi ya Ihefu kwa sababu tuliwapa mapumziko wachezaji wetu baada ya kukamilika kwa mechi za makundi za Ligi ya Mabingwa Afrika tuliporejea kutoka nchini Morocco," alisema.

Kuhusu Mkude, Ahmed alisema amekuwa haonekani uwanjani kwa sababu za kiufundi na wala si nyingine, ila mpaka sasa bado yupo na anaendelea kufanya mazoezi na kikosi hicho.

"Mkude yupo, anafanya mazoezi, hajaonekana kwenye safari hii ya mwisho ya kwenda Morocco kwa sababu za kiufundi kama ambavyo hajaonekana Jimson Mwanuke, hii ina maana kuwa hakujumuishwa kwenye safari, mwalimu ana programu zake, ana wachezaji ambao anawateua kwenye safari na wengine wanabaki, yeye anaamua aende na wachezaji gani ambao watamsaidia.

"Niseme tu kwamba timu kwa sasa inarejea kambini na yeye atakuwa ni mmoja kati ya wachezaji watakaoingia kambini, ina maana bado yupo kwenye kikosi cha Simba," alisema Ahmed.

Mkude ameonekana taratibu anapoteza namba kwenye kikosi cha kwanza cha timu hiyo, ambapo sasa kwenye nafasi ya kiungo wakabaji Simba inategemea wachezaji wawili ambao ni Sadio Kanoute na Mzamiru Yassin.

Kwa sasa wanachama na mashabiki wa Simba huwa hawana amani kama wachezaji hao wote wawili au mmoja tu atakosekana.

Hata hivyo, pamoja na kwamba kuna wakati kiungo mmoja kati ya hao anakosekana, lakini bado chaguo la Kocha Mkuu Oliveira Robertinho limekuwa kwa Erasto Nyoni badala ya

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002